MID WEEK JACKPOT!
TZS. 728,573,060
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumanne Oktoba 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581452
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 3
**Matatani** mauaji ya baba yao kisa kuoa mke wa pili



UKURASA WA 4
**Makamu** wa Rais kukabidhi ndege 2 za mafunzo NIT, Boeing 737



UKURASA WA 5
**Maofisa** ugani 'walia' kupewa pikipiki bila fedha ya mafuta



# Kiharusi tishio

• **Takwimu** za wagonjwa hospitali ya kibingwa zash-tua... *Endelea ukurasa 2*



Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu, Dk. Henry Humba (kushoto), akitoa matibabu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: BMH**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**ADAIWA KUNYONGWA NYUMBA YA WAGENI**
MWANAMKE anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka (32), amekutwa amefariki dunia ndani ya nyumba ya kulala wageni

UKURASA WA 5
**ALIYEDAIWA WAKILI FEKI APANDA KIZIMBANI**
JAMHURI imemfikisha mahakamani Baraka Mukama aliyekamatwa viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi...

UKURASA WA 15
**MUFTI AUNDA TIMU KUCHUNGUZA KUKITHIRI NDOA KUVUNJIKA**
MUFTI Mkuu wa Tanzania, Shehe Abubakar Zubeir ameunda sekretarieti ambayo ameipa jukumu la kufanya utafiti...

KULINDA MAADILI
**Ukinyoa kiduku, kuvaa kimini faini yake 50,000/-**
UKURASA 2

# Moto Kariakoo ngoma ngumu
UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZANUKIA KUKUTANA CAF** UK.24 **KATUNI** UK.6



Kondakta wa daladala linalofanya safari zake Gongolamboto - Mnazi Mmoja akisaidiwa na dereva wake kutoka mkononi mwa abiria aliyecharuka akidai kushushwa Vingunguti kituo kisicho sahihi kwake, baada ya kuzuka mgogoro wakiwa ndani. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Ugonjwa kiharusi tishio

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

DAKTARI bingwa wa upasuaji wa mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Dk. Henry Humba, amesema tatizo la ugonjwa wa kiharusi nchini ni kubwa na hupokea wagonjwa wanne hadi watano kila wiki.

Hospitali hiyo itaanza kutumia teknolojia ya kisasa ya gharama nafuu baada ya madaktari wake kupata mafunzo ya kitaalam ya kutumia teknolojia hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Dk. Humba alisema huduma hiyo ni matibabu ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

"Gharama za matibabu ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika magonjwa ya kiharusi ni nafuu kuliko ya mgonjwa kutumia matibabu ya dawa akiwa ICU," alisema.

Alisema huduma hiyo ni nafuu kwa sababu hutumia muda mfupi mgonjwa kupewa matibabu na hupunguza muda wa kukaa wodini.

Pia, alisema inapunguza muda wa kutumia dawa kwa kipindi kirefu na daktari hutumia muda mchache kwa mgonjwa kumpa tiba.

"Kutumia teknolojia ya kisasa katika upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ina gharama nafuu kuliko mgonjwa kulazwa wodini kwa sababu tiba hii inakwenda kuzibua mishipa ya damu moja kwa moja," alisema Dk. Humba.

Aidha, alisema huduma hiyo itaanza kutolewa katika hospitali ya Benjamin Mkapa ndani ya mwaka mmoja, baada ya madaktari hao kupata mafunzo.

"Vifaa vya utoaji tiba hiyo vipo, lakini hutumika katika matibabu ya moyo, tiba ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu haiko sana kwa sababu wataalam ni wachache tuko takribani 28 nchi nzima," alisema Dk. Humba.

Alisema, tatizo la kiharusi ni kubwa ndio maana serikali iko katika hatua za uanzishwaji wa vyumba vya wagonjwa wa kiharusi (stroke unit).

"Serikali huwashirikisha madaktari hao na kuongeza kuwa vyumba hivyo vitachangia kuongeza uharaka wa kuanzishwa kwa huduma hiyo," alisisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema huduma hiyo inatarajia kuanza ndani ya mwaka mmoja.

Alisema vifaa vyote vipo wakiwamo madaktari bingwa ambao wapo katika mafunzo yanayotolewa kwa ushirikiano wa madaktari kutoka nchini Japani.

**KIHARUSI NI NINI**

Kuna kiharusi cha muda mfupi, ambacho pia huitwa Transient ischemic attack (TIA), ni hali ya mfumo wa neva unaotokea ghafla na hudumu kwa muda mfupi. Hii husababishwa na mishipa ya damu kwenye ubongo kuziba kwa muda mfupi.

Dalili mara nyingi hazidumu zaidi ya saa moja, lakini huweza kudumu hadi saa 24. Dalili za kawaida ni kutoweza kuona, kushindwa kuongea vizuri, udhaifu wa uso, mkono na mguu.

Matibabu hulenga kuzuia hali hii kujirudia au kupata kiharusi kwa kufanya damu iwe nyembamba na kutibu hali ambazo huongeza uwezekano wa kupata kiharusi. Ingawa hali hii haisababishi madhara ya kudumu kwenye ubongo.

Hospitali ya Benjamin Mkapa imekuwa ikishirikiana vizuri na TOKUSHUKAI Medical Group katika tiba ya upandikizaji figo, baada ya mafanikio kuonekana wameanza kushirikiana katika uanzishwaji wa utoaji huduma ya upasuaji ubongo bila kufungua fuvu.

"Tunaishukuru serikali kwa kuruhusu ushirikiano na hospitali za nje katika utoaji huduma za afya ambazo hazipo nchini hii itasaidia kuongeza utalii wa matibabu," alisema Dk. Chandika.

Alisema Wajapani wametoa kifaa ambacho hutumika katika upasuaji wa ubongo bila kutufumua fuvu.

"Tunawashukuru sana Profesa Akio Hydo ambaye ni bingwa mbobezi na mshauri wa huduma za upasuaji mishipa ya damu ya ubongo bila kufungua fuvu kutoka Japan na wenzake kwa ushirikiano wanatoa BMH ili kuhakikisha huduma hiyo inaanza," alisema Dk. Chandika.

Prof. Akio Hydo kutoka Japan alisema wanashirikiana vizuri na BMH kuhakikisha wanaanza kutoa huduma hiyo nchini kwa wagonjwa wenye matatizo hayo.

"Tunafurahi kufanya kazi na BMH tunaishukuru pia serikali kwa kuonyesha ushirikiano," alisema Prof. Hydo.

MKAKATI KULINDA MAADILI

# Ukinyoa kiduku, kuvaa kimini faini 50,000/-

**Na Godfrey Mushi, ARUMERU**

UKINASWA kijiweni bila kazi, faini Sh. 50,000. Ukinyoa 'kiduku', kuvaa mlegezo au suruali iliyotobolewa, pia utatozwa faini hiyo. Ni kati ya sheria mpya zinazotawala kijijini Olevolos.

Ni zao la madai yao kuchoshwa na mmomonyoko wa maadili kijijini kwao, wakazi wake wakipitisha adhabu kisheria inayowabana pia wanaoshinda vijiweni kutwa nzima wakiwa hawana kazi.

Hatua hiyo iliyochukuliwa kijijini huko, Kata ya Kimnya, wilayani Arumeru, mkoani Arusha, imepata baraka za Mwenyekiti wa Halmashauri, Ojung'u Salekwa, akiafiki kutumika kwake, pia Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii, Dk. Dorothy Gwajima, aliyetamka:

"Ninapenda kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wa kijiji cha Olevolos, Emmanuel Ngailuva, kwa kumiliki ajenda ya kupambana na mmomonyoko wa maadili pamoja na Mtendaji wa Kata ya Kimnya. Hakika wamekuwa mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine."

Kwa mujibu wa uamuzi huo wa kisheria kijijini, kuanzia sasa watakaokamatwa vijiweni, watalazimika kulipa faini ya Sh. 50,000 na kama hana atafikishwa mbele ya Baraza la Wazee la Kijiji.

Kuna sheria nyingine ndogo imetungwa katika kijiji hicho; vijana wa kiume hawaruhusiwi kusuka nywele au kunyoa pembezoni mwa kichwa na kuacha katikati (kiduku).

Sambamba na hilo, kuna marufuku ya kuvaa suruali mlegezo, inayoonesha makalio au suruali iliyotobolewa, maarufu 'crazy jeans'.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kimnyaki, Joshua Mollel, faini zake ni Sh. 50,000 au adhabu zingine zitakazopendekezwa na wazee wa kijiji, iwapo mkosaji atakosa fedha za faini.

Wananchi wa Olevolos ambao idadi kubwa ni kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai na Wameru, walipitisha sheria ndogo za kudhibiti vitendo hivyo vya mmomonyoko wa maadili juzi katika mkutano mkuu wa kijiji.

Akisoma sheria hizo na makali yake, Ofisa Mtendaji huyo, pamoja na mambo mengine, alisema zinazuia msichana au mwanamke yeyote kuvaa suruali ya kubana au nguo fupi yenye kuonesha maungo yake, maarufu kimini.

"Wewe mwanamke au msichana, ukibainika faini yake ni Sh. 50,000. Kama hauna hapo, wapo kinamama walioandaliwa, tumeambiwa tuwapelekee.

"Na ni marufuku kijana wa kiume kuonekana amevaa hereni, ukikutwa adhabu yake ni Sh. 50,000. Kama hauna, wazee wamesema tuwaletee.

"Vituo vyote vya bodaboda vilivyopo kijijini wajisajili ofisi ya kijiji, tujue mwenyekiti wao au tujue kwa ujumla viongozi wao, maana kuna bodaboda wanaotumika kwa wizi. Wale waliokufa (alirejea tukio la hivi karibuni) walikuwa bodaboda. Kwa hiyo, sasa tunataka tuwajue rasmi, tuwasajili.

"Vilevile, ni kosa kupika au kuuza pombe haramu ya gongo (moshi) na bangi. Adhabu yake ni kufikishwa mahakamani. Ni kosa kuuza pombe saa za kazi, adhabu yake faini ni Sh. 50,000," alitangaza.

Akifafanua zaidi kuhusu uamuzi wa kutunga sheria hizo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Olevolos, Emmanuel Ngailuva, alisema kuwa pia kuna marufuku ya kulewa au kuuza pombe saa za kazi. Ukikamatwa, adhabu yake ni faini ya Sh. 50,000.

**KAULI HALMASHAURI**

Alipoulizwa kuhusu sheria hizo ndogo kama zina baraka ya kisheria toka Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung'u Salekwa alisema:

"Kila kijiji kina sheria zake ndogo. Kwahiyo, si lazima iwe imepitishwa kwenye Baraza la Madiwani. Ziko za vijiji, lakini wanapaswa kujitazama zisipingane au zisiende kinyume cha sheria za nchi.

"Na mimi pia ningependa kuongeza jambo moja, kwamba lazima tuwe waangalifu katika utekelezaji adhabu hizo. Kwa sababu siyo kila mtu anajua namna ya kumwadhibu mtoto wa mtu.

"Wakati mwingine kuna watu wana chuki binafsi kwenye jamii. Watatumia nafasi hiyo kuhukumu watu ambao walikuwa na visasi nao. Vinginevyo nikwambie hivi, mmomonyoko wa maadili unaendelea kuleta athari kubwa kwa nchi yetu hivi sasa."

**WAZIRI GWAJIMA**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameeleza kufurahishwa na uamuzi wa serikali ya kijiji hicho cha Olevolus kutunga sheria ndogo inayolenga kuzuia mmomonyoko wa maadili na kudhibiti janga hilo katika eneo lao.

Dk. Dorothy katika taarifa yake, amepongeza jitihada hizo za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili, akisema "hatua hiyo ni kubwa kwa jamii yetu kuamua wenyewe kutunga sheria zao kuhusu maadili.

"Kila wakati nimekuwa ninatoa wito kwa viongozi hasa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kubeba ajenda za kusaidia jamii kwenda mbele hasa katika maadili, fursa za kiuchumi na kupinga ukatili."

Waziri Dorothy pia amesema anaishukuru Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kuelekeza masuala ya maadili kujadiliwa katika vikao vya serikali za mitaa.

Ameahidi kuwatembelea wananchi wa Kijiji cha Olevolos ili kuwaunga mkono katika jambo hilo na kuwahamasisha viongozi wengine kuiga mfano kwa kubeba ajenda ya maadili.

Katika taarifa yake, Waziri Dk. Dorothy ametoa wito kwa jamii yote kuendelea kuunga mkono juhudi za viongozi na wataalamu wa serikali ngazi zote katika kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia na watoto na kudhibiti mmomonyoko wa maadili kwa ujumla.

## HABARI KITAIFA

# Matatani mauaji ya baba yao kisa kuoa mke wa pili

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU sita wa familia moja wamekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida kwa tuhuma za kumuua baba yao kwa kile kilichodaiwa kukerwa na kitendo cha kuongeza mke wa pili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, ACP Stella Mutabihirwa aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 30 mwaka huu katika Kijiji cha Kinalilya wilayani Iramba mkoani hapa.

Alisema, watuhumiwa hao ambao hata hivyo hakuwataja majina kwa kuwa uchunguzi bado unaendelea, walimuua Daudi Kitonka (68) kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili wake na kusababisha kutoka damu nyingi.

Kamanda Mutabihirwa alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa kabla ya mauaji kutokea, kulikuwa na ugomvi wa kifamilia baada ya baba kumhamishia nyumbani kwake mwanamke aliyezaa naye watoto wawili nje ya ndoa, kitendo ambacho kilitafsiriwa kuwa ni manyanyaso kwa mke mkubwa.

Katika tukio lingine lililotokea Septemba 9, mwaka huu Kitongoji cha Nkingi, Kijiji cha Misigiri wilayani Iramba, Ester Michael (70), mkazi wa Nkingi, anadaiwa aliuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na begani.

Kamanda huyo alisema kufuatia tukio hilo walikamatwa wawili ambao ni watoto wa marehemu.

Kamanda Mutabihirwa alisema chanzo cha mauaji hayo ni imani za kishirikina ambapo watoto wake wawili wa kuwazaa walikuwa wakimtuhumu kuwa ni mchawi.

Aliongeza kuwa watuhumiwa wengine 57 walikamatwa na mali zinazodaiwa za wizi ambazo ni runinga 14, redio aina sabwoofer nne, Laptop nane, magodoro mawili, power mixer moja, BP mashine, mtambo wa kuvutia shisha na dawa za kulevya aina ya bangi kilo 1.135, pombe ya moshi lita 43 na mirungi gramu 350.

Kufuatia matukio hayo, Kamanda Mutabihirwa aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi na badala yake wawe wanatoa taarifa polisi.

# Moto Kariakoo ngoma ngumu

## ●RC Chalamila aunda kamati kuchunguza chanzo chake

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila ameunda kamati ndogo kuchunguza chanzo cha moto katika Soko la Kariakoo. Itafanya kazi kwa siku saba.

Kamati hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Usalama wa Taifa na wafanyabiashara.

Chalamila alisema katika kikao chake na wafanyabiashara walioathiriwa na tukio hilo jana jijini Dar es Salaam.

Alisema ameunda kamati hiyo kupata majibu sahihi ya chanzo cha tukio, kabla ya hatua stahiki kuchukuliwa, akidokeza eneo mojawapo la chanzo linaweza kuwa hitilafu katika matendo ya kawaida ya mwanadamu.

Alifafanua kuwa moto huo ulisambaa kwa kasi kutokana na vichochoro vilivyounganisha majengo kuzibwa na vibanda vya biashara za mbao.

Chalamila alitumia fursa hiyo kumwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, kuchukua hatua kuondoa vizuizi vyote katika vichochoro vinavyohusu majengo hayo, wakizingatia ramani za mipango miji.

Vilevile, alimwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kudhibiti biashara zisizoendana na taratibu, ili kuepuka vyanzo vya matukio kama ya moto.

Katika utekelezaji huo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mpogolo, mara moja akatoa maelekezo ya marufuku matumizi ya moto wa aina yoyote katika soko hilo.

Alielekeza wanaopika chakula, wapike sehemu nyingine na kupeleka chakula sokoni huko ili kuepuka majanga yatokanayo na moto.

Aliendelea: "Ni marufuku kwa mtu yeyote kupita na moto, madumu ya mishikaki na chipsi. Tumesema hapana moto Kariakoo! Tupike pahala popote tuwaletee chakula Kariakoo.

"Kuna kikao kinafanyika kati ya wakurugenzi wa jiji na manispaa na wafanyabiashara na machinga, kwa lengo la kujipanga vizuri ili soko liwe eneo salama kwa wafanyabiashara na kuvutia wateja kuendelea kununua bidhaa kwenye eneo hili."

Mpogolo alifafanua kuwa katika tukio hilo la moto, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilifanikisha kusalimisha mali nyingi za wafanyabishara.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, alisema anamshukuru Mungu kuwa moto huo haujasababisha kifo kwa wafanyabiashara ingawa umeacha maumivu makubwa kwa watu hao kwa kuteketeza mali zao.

Alisema wataitisha kikao na viongozi wa mkoa kuchunguza chanzo cha moto huo, ili kikomeshwe kwa kuwa unasababisha hasara kubwa kwa wafanyabiashara wa eneo hilo.

"Sasa hivi imeshakuwa mazoea Kariakoo, moto unatokea kila baada ya muda, ndani ya miaka miwili tangu mwaka 2021 kumeshatokea matukio ya moto kama mara tatu, inaathiri sana mitaji ya watu, wengine wanashindwa kuvumilia, inaumiza sana," alisema Mbwana.

IITA Transforming African Agriculture CGIAR

## POSITIONS ANNOUNCEMENT

**The International Institute of Tropical Agriculture (IITA)** is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information about IITA.

IITA is seeking to recruit various nationally recruited staff positions under BioSSA project, to be based in Dar es salaam- Tanzania.

**Position Number 1**
**RESEARCH ASSOCIATE - Ref No. IITA-TZ-2023-NRS-015-DSM**

The Research Associate has the overall responsibility for maintaining, growing, storing and manipulating the microbial strains in the laboratory for field experiments under the BioSSA project. The research Associate will work closely with project staff and will ensure that efficient strain collection management/manipulating, analyses and reporting is done in a timely manner.

This position is based in Dar es Salaam and reports to the Soil Microbiologist.

**Responsibilities:**
- Ensuring microbial collections for use in the project are maintained, stored, grown, and formulated as per the required standards.
- Examination, assessment and characterization of strains used in field trials.
- Extraction, examination and identification of strains used in field trials using dissecting and compound microscopes as well as molecular tools, evaluating influences of crop-soil environment for biostimulant research.
- Ensure microbial mass production for laboratory and field testing.
- Setting up laboratory trials in close collaboration with the project staff.
- Working together and assisting staff and other researchers working in the laboratory and preparation of experimental materials.
- Contribute to developing protocols for assessment of potential products in terms of quality control and quality assurance.
- Establishment of databases (laboratory files, data sheets, logging forms and data entry), keeping them organized, updated, and precise.
- Carrying out inventories and quotations of chemicals, equipment, and laboratory consumables, field samples for laboratory analysis, and maintenance of laboratory equipment
- Coordinating with scientists, other laboratory staff, to ensure that laboratory activities are effectively and efficiently done.
- Supervision of interns/attachment students and perform other duties assigned by the supervisors.

**Criteria for Success**
- Must be able to work independently with minimal supervision.
- Need to participate as a team member in accomplishment of duties.
- Strong attention to detail and maintaining a timely and efficient workflow.
- A positive attitude and strong administrative service orientation.
- Possess excellent interpersonal and communication skills, good judgement, and a high level of respect for confidentiality.
- Ability to work in a multi-cultural environment.
- Critical thinker and curious individual.

**Required Qualifications / Experience**
- MSc degree in soil microbiology and biology molecular technique
- Minimum of three years of working experience
- Experience in soil microbiology research, preferably on topics that are relevant to BioSSA project (fungal collection maintenance, growth of microorganisms, formulation of microbe-based products).
- Proven skills and experience in soil microbiology techniques in the laboratory.
- Familiarity with molecular techniques such as PCR/RFLP and DGGE.
- Computer literacy and statistical data analysis capabilities.
- Fluency in oral and written English.

**Position Number 2**
**FIELD TECHNICIAN - Ref No. IITA-TZ-2023-NRS-016-DSM**

The Field Technician has the overall responsibility for fieldwork activities for the BioSSA Project. The Field Technician works very closely with other research assistants in management of field trials and with the laboratory technicians in preparation of samples for analysis. The position reports to the Soil Microbiologist and is based in Tanzania.

**Responsibilities:**
- Establishment and management of field trials for the project, including application of the biostimulants.
- Collection and processing of samples in the field.
- Preparation of samples (grinding, labelling, storage).
- Perform a variety of routine non-technical duties and assist staff to prepare different activities in the field.
- Perform other related duties to the work described above.

**Criteria for Success**
- Must be able to work independently with minimal supervision, but also participate as a team member in accomplishment of duties.
- Strong attention to detail and maintaining a timely and efficient workflow.
- Possess good interpersonal and communication skills.
- Ability to work in a multi-cultural environment.

**Required Qualifications / Experience**
- BSc in Agriculture or other relevant subject with proven field layout, sample collection and preparation skills.
- At least 3 years of relevant work experience in a closely related field gained in an international organization.
- Computer skills, and ability to learn new applications quickly.
- Ability to work with people and especially farmers, casual labourers and students.

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dae es salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including a cover letter, curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names/addresses of two referees should be addressed to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam and sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to use the position heading reference number as the email subject.

**Closing date is on 16th of October 2023.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

HABARI KITAIFA

# Adaiwa kunyongwa katika nyumba ya kulala wageni

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MWANAMKE anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka (32), amekutwa amefariki dunia ndani ya nyumba ya kulala wageni ya Shivers iliyoko Mtaa wa Kaloleni jijini Arusha, akidaiwa kunyongwa.

Wakizungumzia tukio hilo lililotokea juzi mchana, baadhi ya wakazi wa eneo hilo, akiwamo Saidi Salum, walidai waliona watu wamejaa katika nyumba hiyo ya kulala wageni.

Salum alidai kuwa alipokwenda kushuhudia kilichokuwa kinaendelea baada ya kuona idadi kubwa ya watu, alipata taarifa za mwanamke huyo kuuawa kwa kunyongwa.

"Huyu mwanamke si mgeni, tunamfahamu, maana hili ni eneo lake la kazi. Alikuwa ana... (alitaja neno lenye maana ya biashara isiyoruhusiwa kisheria) kila siku. Hata hapa Shivers ni mwenyeji, tunasikitika sana," alisema.

Shuhuda mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Kiu, alisema matukio kama hayo kwa Arusha ni mengi kwa sasa, hivyo aliomba serikali kuyafanyia kazi, ili wahusika wachukuliwe hatua kali na kuyakomesha.

Anna John alisema amepokea kwa masikitiko kifo cha mwenzao kwa kuwa hakuwa na ugomvi na mtu na alikuwa kazini.

Alidai kuwa kuna kijana alifika nyumba hiyo ya kulala wageni asubuhi na ilipofika mchana, alishangaa kumwona kijana huyo anakimbia akiwa na nguo ya ndani tu.

"Baada ya kuona amekimbia, waendesha pikipiki na vijana wengine walipo eneo hili walishirikiana kumkimbiza na kumkamata eneo la Mnara wa Mwenge, mita chache kutoka hapa kisha kumkabidhi kwa polisi waliokuwa tayari wamefika eneo la tukio," alidai.

Anna aliendelea kusimulia kuwa polisi walipofika katika nyumba hiyo ya wageni, waliingia katika chumba alimokuwa mwanamke huyo na kukuta haja kubwa imetapakaa kitandani na umauti ulikuwa umeshamkuta mwanamke huyo. Walibeba mwili wake na kuondoka nao.

Hassan Hamis alidai alimwona kijana huyo akiingia katika nyumba hiyo na baada ya muda alisikia kelele ndani ya chumba hicho zilizoashiria mzozo na ilipofika mchana, aliona kijana huyo anatoka kwa kukimbia akiwa amevaa nguo ya ndani tu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alithibitishwa kuwa na taarifa za tukio hilo katika nyumba ya kulala wageni ya Shivers.

"Kwa sasa wataalamu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mount Meru) wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo ili tujue kwa hatua zaidi," alisema.

Kamanda Masejo alisema hawawezi kutaja jina la marehemu na mtuhumiwa kwa sasa mpaka uchunguzi utakapokamilika.




Mwanafunzi katika Mtaa wa Stakishari, Kata ya Ukonga Manispaa ya Ilala, akipita chini ya karavati baada ya kivuko kujengwa eneo la mbali kutokana na ujenzi wa reli ya mwendokasi. Eneo hilo hutumiwa na wakazi wake kama njia ya kutokea upande wa pili. **PICHA: SALAMA RINGO**.


# Bonite Bottlers Limited

**P.O.Box 1352,MOSHI, Email bbl@bbl.co.tz, Tel:+255 27 2754422-4 SHIRIMATUNDA TANZANIA**

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Position: SALESMAN/SALES LADY**

Bonite Bottlers Limited has an exciting opportunity in Sales & Marketing department. We are looking for talented individuals with relevant skills and qualifications in Sales for a Salesman/lady position.

**Qualification & Requirements**

- Applicant should be a holder of Diploma in Sales & Marketing, Business Administration or related field.

**Key skills & Abilities:**

- Skills and knowledge of customer service and support
- Ability to seek out and develop new business and maximize all possible opportunities to increase sales.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self-motivated, target-oriented and a good team player
- Strong communication and interpersonal skills.

**Mode of Application:**
Interested candidates are invited to submit their resume and a cover letter detailing their relevant experience and explaining why they are the right fit for the Salesman/lady position.

Please send your application to the undersigned, to reach him not later than **6th October 2023.**

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**


# Mpango kukabidhi ndege mbili NIT mafunzo ya anga

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kukabidhi ndege mbili za injini moja aina ya Cessna Skyhawk 172 kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kutoa fursa kwa chuo hicho kufundisha mafunzo ya anga hasa urubani.

Ndege aina ya Cessna Skyhawk ndiyo ndege maarufu zaidi zenye injini moja ambazo zinatengenezwa na Kampuni ya Marekani ya Textron Aviation. Zinatajwa ni ndege bora zaidi kwa mafunzo ya anga.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa serikali itaendelea kuijengea uwezo NIT ili kutoa marubani na wafanyakazi katika sekta ya usafirishaji.

Prof. Mbarawa alisema kuwa mwaka 2021, serikali iliiwezesha NIT kununua ndege mbili ambazo zitatumika kwa mafunzo ya urubani na mafunzo mengine ya usafiri wa anga.

Prof. Mbarawa alidokeza kuwa masomo ya urubani ambayo kwa sasa yanatolewa nje ya nchi kwa ada ya zaidi ya Sh. milioni 300, sasa yataanza kutolewa nchini kwa ada ndogo.

"Serikali itaendelea kuisaidia NIT ili kuweka nguvu zaidi katika kufundisa rasilimali watu katika sekta ya usafirishaji," alisema Waziri Mbarawa.

Naibu Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi wa Wizara ya Uchukuzi, Biseko Chiganga, alisema serikali imewapa NIT eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa ajili ya kujenga hanga litalotumika kwa mafunzo ya anga ikiwamo urubani.

"NIT itajenga shule ya mafunzo ya anga katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Kwa wakati huu ambao wanasubiri kukamilika kwa ujenzi huo, watakuwa wanatumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) kwa mafunzo ya vitendo," alisema.

NIT pia ni mnufaika wa Mradi wa Ujuzi wa Afrika Mashariki wa Mabadiliko na Utangamano wa Kikanda (EASTRIP) uliozinduliwa Addis Ababa, Ethiopia na nchi tatu zinazoshiriki katika mradi ho; Tanzania, Ethiopia na Kenya.

Kupitia mradi huo, NIT ilipokea dola za Marekani milioni 21.25 (Sh. bilioni 50) kama msaada wa kifedha kutoka Benki ya Dunia (WB) katika kusaidia masomo ya usafiri wa anga.

Mradi huo unasaidia uundaji wa programu maalum za Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi (TVET) na mafunzo ya muda mfupi ya kiwango cha cheti kinachotambuliwa na tasnia na utalenga sekta za kipaumbele za kikanda katika usafirishaji, nishati, utengenezaji na ICT.

# Aliyedaiwa wakili feki apandishwa kizimbani

**Na Kulwa Mzee**

JAMHURI imemfikisha mahakamani Baraka Mukama aliyekamatwa viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Mei, mwaka huu, kwa tuhuma za kufanya kazi ya uwakili bila kuwa na sifa.

Mukama alipandishwa kizimbani jana na kusomewa mashtaka mawili mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swallo.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili wa Serikali, Judith Kyamba, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, mshtakiwa anadaiwa kumzuia askari polisi mwenye namba J. 515 PC Mubaraka Abdallah kufanya kazi yake.

Alidai kuwa Mei 23 mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mshtakiwa alimzuia mtumishi wa umma kutekeleza majukumu yake ya kumkamata Harid Rajabu.

Wakili Judith alidai katika shtaka la pili, siku hiyo mshtakiwa, akiwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Romuli Mbuya, alimwakilisha mshtakiwa na kujitambulisha kuwa ni wakili mwenye namba ya usajili 4696 huku akiwa anafahamu si kweli.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa alikana kutenda makosa hayo na upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa shauri hilo umekamilika, hivyo uliomba tarehe nyingine ya kumsomea hoja za awali.

Mahakama ilikubali kumpa dhamana kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili waaminifu watakaotia saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni moja kila mdhamini.

Mshtakiwa alitimiza masharti ya dhamana. Yuko nje kwa dhamana. Kesi iliahirishwa hadi Oktoba 16 mwaka huu kwa ajili ya kusomewa hoja za awali.

Mei 23 mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mshtakiwa alizua tafrani kwa kuzuia askari wasimkamate mshtakiwa Harid Rajabu aliyekuwa ameachiwa na mahakama hiyo kwa kifungu namba 225 cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

Mshtakiwa alifanikiwa kuwazuia wakiwa ndani ya mahakama, walikimbia, lakini wakakamatiwa nje ya lango la mahakama pamoja na wakili wao huyo aliyekuwa akizuia askari kufanya kazi yao.

# Maofisa ugani walia kukosa mafuta, fedha za matengenezo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADA ya serikali kuwapatia maofisa ugani pikipiki kwa ajili ya kuwafikia wakulima kwa urahisi, maofisa hao katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wamedai hawana mafuta na fedha za matengenezo.

Wamesema hali inayowafanya washindwe kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Kwa mujibu wa utaratibu, maofisa hao wanatakiwa kuwekewa mafuta katika pikipiki zao kupitia Mfuko wa Halmashauri kuwawezesha kuwafikia wakulima shambani na kuwapatia elimu ya kulima kisasa mazao ya chakula, biashara na mikunde, lakini kukosekana kwa mafuta hayo kunasababisha wakulima kukosa elimu ya kulima kisasa.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana Ofisa Kilimo Kata ya Kinamapula Halmashauri ya Ushetu, Fadhili Kadyue, kuhusu uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara baada ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwapatia pikipiki maofisa hao, alisema wanashindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na kutokupatiwa mafuta.

Alisema wamewapatia vyombo hivyo vya usafiri, lakini hawajawapatia fedha za matengenezo na mafuta ya kuwawezesha kuwafikia wakulima, hali inayoathiri mzunguko wa kuwafikia wakulima wote na kuwaelimisha kulima kisasa kulingana na maeneo yao ya kilimo.

"Kwa sasa ninalazimika kutumia mikutano ya hadhara inayoitishwa na diwani, mihadhara ya kidini na vikundi vya kuweka na kukopa vilivyoko katika kata hasa pale vinapokutana, ninafika na kutoa elimu ya kulima kisasa, baadhi ya vikundi kipindi cha nyuma tuliviunda wenyewe," alisema Kadyue.

Alisema kata hiyo ina vijiji sita vya Kinamapula, Kalama, Ilevye, Hongwa, Butibu na Kasomela na kwa wiki anahakikisha anavitembelea vyote kulingana na mafuta atakayokuwa nayo. Anafafanua kuwa ananunua mafuta kwa kutumia mshahara wake.

Aliomba serikali kuliangalia suala hilo ili wawafike zaidi wakulima kuwasaidia kulima kisasa na kuongeza mavuno yao.

Mmoja wa wakulima wa Kinamapula, John Makonda alisema maofisa hao hawawafikii ipasavyo kwa kile wanachoeleza kuwa ni ukosefu wa mafuta, hali ambayo inawafanya waendelee kulima kwa mazoea na kupata mavuno kidogo.

Diwani wa Kinamapula, Sharifu Samweli, alisema wakulima wengi wanalima kienyeji kutokana na kutokufikiwa kwa wakati na maofisa ugani. Katika vikao vyao vya Baraza la Madiwani hawajawahi kupata ripoti yoyote ya halmashauri kuwapatia mafuta na matengenezo kila mwezi ya pikipiki.

Alisema baadhi ya maofisa kilimo wamekuwa wanatumia fedha zao binafsi kujaza mafuta katika pikipiki hizo, hali inayopunguza ufanisi wa kazi, hasa kuwatembelea wakulima.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Ushetu, Mapenzi Mshana, alithibitisha kutowapatia mafuta na matengenezo ya pikipiki maofisa ugani wake na kuwataka kuwa wavumilivu katika kipindi ambacho wanaendelea kujinunulia mafuta kwa fedha zao wakati serikali kuwanunulia mafuta ukiendelea kuwekwa sawa.

Alisema kiutaratibu wanapaswa kupewa mafuta kila mwezi si chini ya lita mbili sambamba na matengenezo yake na halmashauri nyingine zinafanya hivyo kwa maofisa ugani wake.

"Kabla ya kupatiwa pikipiki hizi walifanya kazi vyema na waliwafikia wakulima kwa wingi, hivyo wasikate tamaa ya kazi kwa ukosefu wa mafuta. Utaratibu ukishawekwa sawa wataanza kupatiwa," alifanua.

---

ZRA ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

**MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR**

## TAARIFA KWA UMMA

### KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO

**Zanzibar, 30 Septemba, 2023.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), inaufahamisha umma kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78) kuhusu viwango maalum vya kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024 kwa mujibu wa kifungu cha 7A (1) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam.14 ya Mwaka 2008.

Tangazo la Kisheria la kutoza kodi ya majengo kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, **LIMESAMEHE KUTOZWA KODI YA MAJENGO kwa MAJENGO YA MAKAAZI yasiyo ya Ghorofa.**

Majengo yafuatayo yatatakiwa kulipa kiasi maalum cha kodi kama ilivyoainishwa katika Jadweli hapa chini:

| SN | AINA YA JENGO | KIASI CHA KODI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Majengo ya ghorofa ya makaazi au kondominiam | Tzs. 10,000/= kwa kila ghorofa au Jengo (Unit) |
| 2. | Majengo ya biashara yenye ghorofa | Tzs. 50,000/= kwa ghorofa |
| 3. | Majengo mengineyo ya biashara | Tzs. 50,000/= |
| 4. | Majengo ya hoteli:<br>(a) Hoteli ya nyota tano<br>(b) Hoteli ya nyota nne<br>(c) Hoteli ya nyota tatu<br>(d) Hoteli ya nyota mbili<br>(e)Hoteli ya nyota moja<br>(f) Hoteli nyenginezo | <br>Tzs. 500,000/=<br>Tzs. 400,000/=<br>Tzs. 300,000/=<br>Tzs. 200,000/=<br>Tzs. 100,000/=<br>Tzs. 50,000/= |

**2.0 MUDA WA KISHERIA WA KULIPIA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya Mwaka 2008, kiasi chote cha kodi ya majengo kwa mwaka kinapaswa kulipwa kabla au siku ya tarehe **30,Septemba** ya kila mwaka, na si zaidi ya tarehe **30, Juni** ya mwaka unaofuata.

**3.0 KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha Sheria kilichotajwa hapo juu, kodi ya majengo inalipwa kabla au siku ya tarehe 30, Septemba, 2023. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba, viwango vya kodi ya majengo vimeanzishwa hivi karibuni chini ya alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), hivyo basi hii ni sababu ya msingi na yenye kutosheleza kuongeza muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024.

Kwa muktadha huo, na kwa mujibu wa kifungu cha 10 (2) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008, tarehe ya mwisho ya kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024, imeongezwa kutoka siku ya tarehe ya 30 Septemba, 2023 hadi siku ya tarehe 30 ya Novemba, 2023.

**4.0 MADHARA YA KUTOLIPA KODI YA MAJENGO KWA WAKATI:**

Mmiliki yeyote wa jengo lililo miongoni mwa majengo yaliyoorodheshwa katika Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), anapaswa kulipa kodi ya majengo kabla au siku ya tarehe 30, Novemba,2023, ili kuepuka adhabu kama ilivyotolewa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi, Na. 7 ya 2009.

**5.0 HITIMISHO:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar inawataka wamiliki wa majengo husika kutumia vizuri nyongeza ya muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo katika kutimiza wajibu wao.

Wakati huo huo, ZRA, itaanza kampeni ya uhamasishaji na utaratibu wa ulipaji kodi hii kwa wamiliki wote wa majengo husika ili kuongeza uwajibikaji wa hiari kabla ya tarehe ya mwisho ya kulipa kodi. ZRA inawahakikishia wamiliki wote wa majengo kuendelea kuchukua hatua za kisheria zinazofaa katika kurahisisha ulipaji kodi ya majengo kwa hiari.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

Yusuph Juma Mwenda
**Kamishna Mkuu**

SLP 2072,
SLP 163 (P)

255-24-245255 (
255-24-2233041

www.zanrevenue.org
1 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi, Zanzibar
262 Barabara ya Chake-Wete, 74206 Wara, Kusini Pemba, Zanzibar (P)

zra@zanrevenue.org

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Majanga yakabiliwe kabla ya kuleta madhara

**MATUKIO** ya majanga ya moto kutokea katika maeneo ya biashara na makazi ya watu, yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara na yanapotokea jinsi ya kuyakabili huleta ugumu kutokana na sababu kadhaa.

Matukio haya huleta athari kubwa kutokana na waokoaji ambao ni kikosi cha Zimamoto kupata changamoto hasa ya miundombinu.

Eneo la kibiashara la Kariakoo ambalo ni maarufu kwa biashara limekuwa na msongamano mkubwa wa majengo ambayo majanga yanapotokea ni vigumu kukabiliana nayo.

Kwa Kariakoo hii ni mara ya pili kutokea kwa tukio la moto kuteketeza majengo na mali za mamilioni ya fedha.

Tukio la kwanza lilikuwa la Soko la Kariakoo ambalo ni maarufu na kutegemewa kwa biashara mbalimbali zikiwamo bidhaa za vyakula na nyingine nyingi.

Wakati soko hilo likiendelea kujengwa kutokana na janga la moto, eneo hilo hilo tena moto umeteketeza maduka zaidi ya 900 ya wafanyabiashara na kuwaacha katika hali ya sintofahamu.

Wafanyabiashara wengi waliwekeza mitaji yao hapo wakitegemea kujikomboa katika umaskini, lakini moto umewarudisha nyuma.

Kuna waliokopa pesa benki ili kuwekeza mitaji kwenye biashara wakitegemea kupitia uwekezaji huo watarudisha mikopo hiyo bila tatizo.

Wengine ni wastaafu ambao baada ya kulipwa kikokotoo chao wameamua kuwekeza kwenye biashara ya maduka, lakini moto umezima ndoto na kuwaacha wasijue cha kufanya.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alipotembelea eneo hilo na kuangalia jinsi maduka yalivyosongamana mpaka sehemu za vichochoro ambazo ziliachwa kwa sababu ya kuacha njia ya kupita, zimezibwa kwa kujengwa mabanda.

Wakati maduka hayo yanajengwa mpaka kuziba barabara, wahusika na uangalizi wa mipango miji wapo, lakini hali hiyo imeachwa na kufikia hatua ya kutokuwa na njia na badala yake kujaa maduka ya biashara.

Kikosi cha Zimamoto mara nyingi kunapotokea janga kama hilo, sababu kubwa wanayotoa kushindwa kuokoa majengo yanayoteketea ni kukosekana kwa njia ya kuwawezesha kufikia sehemu husika na kudhibiti moto.

Tatizo hili la kuzibwa kwa miundombinu ya barabara, linazungumzwa mara kwa mara, lakini janga linapopita kila kitu kinasahaulika, mpaka linapotokea lingine, kunatolewa sababu ambazo kama zingetatuliwa mapema majanga hayo yangeweza kudhibitiwa.

Hasara inayojitokeza ni kubwa na wengine hushindwa kubeba mzigo wa mawazo na kupoteza uhai kutokana na msongo.

Chakushukuriwa ni kwamba janga hilo halijasababisha vifo vya watu zaidi ya kuteketeza maduka na mali zilizokuwamo ndani.

Kama tukio hilo lingetokea kipindi ambacho Kariakoo inakuwa na msongomano wa watu wanaotafuta bidhaa, basi ingekuwa inaongolewa habari nyingine ya vifo.

Hili ni funzo lingine la kujifunza kujiepusha na majanga kwa kuweka miundombinu inayopitika vizuri.

Tatizo sio janga la moto pekee, kuna mafuriko ambayo pia husababisha hasara na hatari kwa usalama wa wafanyabiashara na wakazi wa eneo hilo.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), imeshatabiri kutarajiwa mvua ya El-Nino, kama kusipokuwa na maandalizi ya kujihami mapema basi itarajiwe majanga kama hayo kutokea na sababu zitakuwa zilezile.

Wanaojenga kiholela kwenye eneo hilo wadhibitiwe mapema, wasiachwe mpaka tatizo linapotokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Watoto mazingira magumu wasaidiwe ili wasome

**KATIKA** maeneo ya mijini, imekuwa kama jambo la kawaida kukuta watoto wadogo wenye umri wa kwenda shule wakiwa kandokando ya barabara kuomba msaada na fedha.

Ingawa zimekuwapo jitihada za kuwarejesha kwao, ili kuungana na familia zao, juhudi hizo hazijazaa matunda, hali ambayo inaonyesha kuwa kuna haja ya kuongeza mbinu zaidi za kukabiliana na tatizo hilo.

Mikakati hiyo ni ile iliyowahi kufanywa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima ya kukutana na watoto katika baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam.

Imepita miaka mitatu sasa alipofanya ziara ya kuwatembelea watoto hao Ubungo na kuzungumza nao na kuelezwa changamoto wanazokutana nazo huku baadhi wakitamani kurudi kwao.

Hata hivyo, ni kama haya yamepita na sasa kuna haja ya kuja na njia bora zaidi ya kusaidia waweze kusoma, nayo ni jamii kuungana na harakati za kuwakusanya na kuwarudisha kwao ili waache maisha ambayo hayana jibu la hatima ya maisha yao.

**Utaratibu wa kuwaondoa mitaani ulioanzishwa na serikali ungekuwa wa kudumu kwa kushirikisha wadau wa elimu wakiwamo walimu, wazazi na walezi, ili uweze kuwa na matokeo chanya.**

Utaratibu wa kuwaondoa mitaani ulioanzishwa na serikali ungekuwa wa kudumu kwa kushirikisha wadau wa elimu wakiwamo walimu, wazazi na walezi, ili uweze kuwa na matokeo chanya.

Kimsingi, watoto wenye umri wa kwenda shule, wanatakiwa wawe darasani, lakini inasikitisha kuona baadhi yao wakirandaranda kandokando ya barabara au mitaani wakifanya kazi ya kuomba msaada.

Bila kuwapo jitihada zaidi za kuwasaidia warudi kwao au wapelekwe kwenye vituo maalum, inaweza kuwa vigumu kupata elimu na hivyo, kushindwa kutimiza ndoto zao za baadaye walizojiwekea.

Katika makundi hayo ya watoto wa mitaani, wanaweza wakawamo viongozi, wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye, hivyo bila kuwasaidia, wanaweza kujikuta wakiwa wahuni wa baadaye.

Wapo baadhi ya watoto waliowahi kutoa sababu mbalimbali ambazo zilizowafanya wakimbie kutoka nyumbani kwao, ikiwamo migogoro ya kifamilia, ambayo ni wazi ziko chini ya uwezo wa familia zenyewe.

Waliwahi kutoa sababu hizo mbele ya Waziri Dk. Doroth Gwajima, jijini Dar es Salaam wakitamani kurudi kwao ili waungane na wazazi wao.

Nadhani njia nzuri ya kusaidia waweze kusoma, ni kuungana na serikali katika harakati za kuwakanya na kuwarudisha kwao ili waache maisha ambayo yanatishia maisha yao.

Utaratibu wa kuwaondoa mitaani ulioanzishwa na serikali ungekuwa wa kudumu ili uweze kuwa na matokeo chanya, kwani kama umesimama tangu ulipoanzishwa mwaka juzi.

Ninaamini utaratibu wa kukutana na watoto ili kujua chanzo cha wao kukimbia kutoka nyumbani kwao na kulazimika kuishi mitaani, ulikuwa njia mbadala na mbinu nzuri ambayo ingesaidia kumaliza tatizo.

Kwa sababu muda mrefu wamekuwa wakiondolewa mitaani, hasa ya Dar es Salaama, lakini baadaye wanarudi, hivyo iwapo wadau watashirikishwa kwa ajili ya kutoa taarifa inaweza kuwa rahisi kupata habari zao mbalimbali.

Jamii inaweza kushiriki kwa kutoa taarifa sahihi za walipo watoto hao ili kusaidia kuwapata kila kona ya nchi na kuwarudisha kwao, wapate elimu, kwani inawezekana wengi wakakosa kusoma.

Iwapo hilo litafanyika, linaweza kuleta mafanikio ya kuwaondoa mitaani na kusaidia wale waliokimbia kutoka kwao wakiwa wanasoma, ili waandaliwe utaratibu wa kuendelea na masomo.

Hivyo, serikali ingeufanya utaratibu wa kuwaondoa mitaani kuwa endelevu kwa kushirikisha jamii ili kupata taarifa sahihi za walipo na hata chanzo cha watoto kukimbia kwao kitafutie ufumbuzi wa kudumu.

Watoto hao ndio taifa la sasa wanaoanza kuandaliwa leo, hivyo ni vyema wasaidiwe kupata elimu ambayo itawawezesha kulisaidia taifa lao kupitia taaluma watakazosoma badala ya kuandaliwa kuwa mzigo wa baadaye utakaokosa wa kuubeba.

## Mtego wanasa watuhumiwa wizi wa ng'ombe mradi wa BBT

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

KUTOKANA na wizi wa ng'ombe katika shamba la mifugo la serikali (BBT) Kampasi ya Mabuki wilayani Misungwi mkoani Mwanza, Mkuu wa Wilaya hiyo, Paul Chacha ameweka mtego na kufanikiwa kukamata watu watatu akiwamo mfanyakazi wa shamba hilo, wakituhumiwa kwa wizi wa ng'ombe tisa.

Waliokamatwa kwa tuhuma hizo ni Daudi Msobi, Shileta Paul na Boniphace Kileleju huku serikali ikiagiza vijana wengine 60 wanaoshiriki katika mradi huo kuhojiwa kuhusu wizi huo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kukamatwa kwa watu hao, Mkuu wa Wilaya Chacha alisema amekuwa anapokea taarifa ya kupotea ng'ombe katika shamba hilo katika mazingira yenye utata. Mifugo iliyoko shambani huko haichangamani na mingine.

"Awali walipotea ng'ombe watatu, tukaona kama kuna mchezo unaofanyika. Ikabidi tuweke mtego, siku ya jana (juzi) ukazaa matunda baada ya kufanya sensa na kubaini kupotea kwa ng'ombe sita. Tulifuatiliwa na kubaini mifugo hilo iliko," alisema Chacha.

Alisema kuwa baada ya kuchukua mifugo hiyo, wanabadilishwa kwa kuwavua baadhi ya alama walizonazo ikiwa ni pamoja na heleni kisha kuwauza kwa wanunuzi katika maeneo mbalimbali wilayani Misungwi ambao hawawezi kuwatofautisha.

Aliongeza kuwa mitego hiyo ilibaini wezi hao wanashirikiana na wenyeji katika shamba hilo akiwamo mtumishi shambani ambaye amekamatwa na adaiwa kufanya hivyo mara kwa mara.

"Kingine katika mradi huu, wapo wanafunzi 60 ambapo kila mwanafunzi ananufaika na ng'ombe, wanafundishwa namna ya kuwafuga, kuwanenepesha kisha kutafuta masoko lakini ng'ombe hao wamekuwa wakiibwa mchana wakati wa kuchunga, hivyo na wanafunzi hawa wanachunguzwa juu ya wizi huu," alifafanua.

Alisema katika mradi huo, ulinzi upo wa kutosha lakini kutokana na wezi hao kuhusika katika mradi moja kwa moja wanatekeleza matukio nje ya eneo hilo, hasa wakati wa kuwachunga.

Vilevile, alieleza kuwa serikali bado inaendelea na upelelezi mkali ili kumbaini mnunuzi kinara wa ng'ombe hao, akiwahakikishia waandishi wa habari kuwa ndani ya siku mbili atakuwa amekamatwa.

Meneja wa Mradi wa BBT Kampasi ya Mabuki, Jacob Chacha alieleza kuwa baada ya ng'ombe hao kukosekana wakati wa sensa ya jioni, walifuatilia na kukuta wakiuzwa katika eneo la Misasi na watuhumiwa waliokamatwa ni vijana pamoja na mmoja wa wafanyakazi wa shamba hilo.

"Tayari wamehojiwa na polisi na kukili kuhusika na wizi huo wa ng'ombe sita. Tunawashukuru kuwa wanaweza kuwa wahusika pia wa wizi wa ng'ombe wengine watatu waliopotea kipindi cha nyuma," alisema Jacob.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (wa pili kulia), akipokea kadi yake ya 'TemboCard' kutoka kwa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu na Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023 iliyofanyika katika tawi la benki hiyo la Azikiwe jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Ofisa Mkuu wa Uendeshaji Benki ya CRDB, Bruce Mwile (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja CRDB, Yolanda Uriyo (wa pili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### MATUMIZI BILIONI 3.93/-

## Waziri aagiza vigogo wasimamishwe kazi

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameagiza kusimamishwa kazi watumishi watatu wa hospitali ya wilaya na vituo vya afya vya Mollo na Matanga katika Manispaa ya Sumbawanga ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Nteghenjwa Hossea, ilibainisha kuwa Waziri Mchengerwa amechukua uamuzi baada ya kufanyika ukaguzi na ufuatiliaji maalum wa ujenzi katika vituo hivyo vya afya na hospitali ya wilaya.

Watumishi hao ni aliyekuwa Mganga Mkuu wa Manispaa, Dk. Archie Hellar, aliyekuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi, Denis Eliakim na aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Obedi Mwakalinga.

"Matokeo ya ukaguzi na ufuatiliaji huo yamebainisha miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji ilipokea Sh. bilioni 3.99 na jumla ya Sh. bilioni 3.93 zimetumika sawa na asilimia 98.56 ya fedha zote zilizopokewa kutoka serikalini," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Ilibainishwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa katika ukaguzi wa matumizi yaliyofanyika, kumebainika kuwapo kasoro mbalimbali zinazohusiana na ukiukwaji taratibu za fedha na ununuzi, usimamizi hafifu wa miradi uliochangia kutokamilika kwa ujenzi wa hospitali ya wilaya na kukosekana ushirikishwaji.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kutokana na hali hiyo, Waziri Mchengerwa ameelekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchukulia hatua dhidi ya watumishi wote waliobanika kusababisha changamoto kwenye miradi hiyo akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Jacob Mtalitinya ambaye kwa sasa amehamia taasisi nyingine.

Mbali na kutoa maagizo hayo, Waziri Mchengerwa pia amemwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuchukualia hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya watumishi wote waliohusika kama walivyobainishwa katika matokeo ya ukaguzi na ufuatiliaji maalum kwa kila eneo lenye kasoro.

Pia, ameagiza kurejeshwa mtumishi yeyote aliyetajwa katika ripoti ya ukaguzi huo ambaye kwa sasa amehamia ofisi nyingine na achukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

Agizo lingine ni kuhakikisha vifaa vyote vya ujenzi vilivyohamishiwa kwenye miradi mingine, vinarejeshwa kwenye eneo la mradi.

Lingine ni kuhakikisha kamati za ujenzi zinajengwa uwezo na kuwezeshwa kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu katika miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa kutumia wataalamu wa ndani.


Agizo lingine la waziri huyo ni kuhakikisha viongozi na kamati zinazingatia kikamilifu taratibu za fedha, ununuzi na thamani halisi ya fedha katika ujenzi wa miradi ya maendeleo. Waziri Mchengerwa pia ameagiza kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kuviwezesha vitengo vya ukaguzi wa ndani katika halmashauri zote nchini kutekeleza majukumu yake kikamilifu na ushauri na mapendekezo yake yanafanyiwe kazi.

Agizo lingine ni kuhakikisha Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inaandaa mpango kazi wa ukamilishaji wa majengo saba ya awali katika hospitali ya wilaya na kuwasilishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Waziri huyo ameonya kuwa kuanzia sasa mtumishi yeyote wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakayetenda kosa katika halmashauri hiyo na kuhamishwa ama kustaafu, atarejeshwa kwanza katika kituo chake cha kazi cha awali alichotenda kosa hilo na kuchukuliwa hatua za kisheria.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# KIBO SEED COMPANY LTD

## BEI YA BIDHAA MWAKA 2023

| | 2KG | |
|---|---|---|
| MBEGU ZA MAHINDI | BEI YA JUMLA | BEI YA REJAREJA |
| H 513 | 10,500 | 12,500 |
| H 519 | 10,500 | 12,500 |
| H 614 | 10,500 | 12,500 |
| H625 | 10,500 | 12,500 |
| H628 | 10,500 | 12,500 |
| DH04 | 10,500 | 12,500 |

| | 1KG | |
|---|---|---|
| MBEGU ZA ALIZETI | BEI YA JUMLA | BEI YA REJA REJA |
| Kenya Fedha Sunflower | 8,000 | 8,500 |

| BEI ZA MBOGA MBOGA | 10GM | 25GM | 50GM | 100GM | 250GM | 500GM | 1KG |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MBEGU ZA KAWAIDA (OPV) | | | | | | | |
| BIRINGANYA (EGG PLANT) | | | | | | | |
| Eggplant Black Beauty | 1,700 | 4,000 | 7,000 | 14,000 | 31,000 | 62,500 | 123,500 |
| Eggplant Long Purple | 2,500 | 4,500 | 8,000 | 15,500 | 36,500 | 72,000 | 133,000 |
| (Ngogwe) DB3 | 1,500 | 2,500 | 4,000 | 7,000 | 16,000 | 29,000 | 52,000 |
| (Ngogwe)TENGERU WHITE | 1,500 | 2,500 | 4,000 | 7,000 | 16,000 | 29,000 | 52,000 |
| | | | | | | | |
| KABICHI | | | | | | | |
| COPENHAGEN MARKET | 1,500 | 2,500 | 3,500 | 6,000 | 13,000 | 23,000 | 44,000 |
| GLORY OF ENKHUIZEN | 1,500 | 2,500 | 3,500 | 6,000 | 13,000 | 23,000 | 44,000 |
| CHINESE CABBAGE MICHIHILI | 1,200 | 1,600 | 3,000 | 4,300 | 10,000 | 16,000 | 30,500 |
| CAULFLOWER SNOW BALL | 2,500 | 5,000 | 10,500 | 19,500 | 48,000 | 95,000 | 185,500 |
| | | | | | | | |
| HOHO (CAPSICUM) | | | | | | | |
| CALIFONIA WONDER | 2,500 | 5,000 | 10,200 | 21,000 | 52,000 | 103,000 | 210,500 |
| | | | | | | | |
| CARROT | | | | | | | |
| CARROT NANTES | 1,200 | 2,200 | 4,000 | 7,500 | 16,800 | 32,500 | 55,000 |
| CARROT KURODA | 2,000 | 3,000 | 5,500 | 10,000 | 21,500 | 42,000 | 80,000 |
| | | | | | | | |
| BAMIA (OKRA) | | | | | | | |
| CLEMSON SPINELESS | 800 | 1,300 | 2,000 | 3,500 | 5,500 | 9,500 | 19,000 |
| PUSA SAWANI | 800 | 1,300 | 2,000 | 3,500 | 5,500 | 9,500 | 19,000 |
| | | | | | | | |
| VITUNGUU(ONION) | | | | | | | |
| ONION RED BOMBAY | 1,500 | 2,500 | 4,500 | 8,000 | 18,000 | 35,500 | 70,000 |
| RED CREOLE | 2,000 | 3,500 | 6,500 | 12,000 | 26,000 | 46,000 | 91,000 |

| AINA | 10GM | 25GM | 50GM | 100GM | 250GM | 500GM | 1KG |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MBEGU ZA KAWAIDA (OPV) | | | | | | | |
| NYANYA (TOMATOES) | | | | | | | |
| CAL J | 2,000 | 3,500 | 6,000 | 11,500 | 27,000 | 52,000 | 78,000 |
| TENGERU 97 | 2,000 | 3,500 | 6,500 | 13,000 | 29,000 | 58,000 | 90,000 |
| MWANGA | 3,000 | 6,000 | 12,000 | 22,500 | 53,000 | 102,000 | 200,000 |
| TOMATO ROMA VF | 2,000 | 4,000 | 7,500 | 14,500 | 31,000 | 62,000 | 123,000 |
| TOMATO RIOGRAND | 3,000 | 5,500 | 11,000 | 21,500 | 52,000 | 101,000 | 199,000 |
| | | | | | | | |
| TIKITI MAJI (WATERMELON ) | | | | | | | |
| CRIMSON.SWEET | 2,500 | 4,500 | 8,500 | 17,000 | 40,000 | 75,500 | 119,000 |
| SUGAR. BABY | 2,000 | 3,000 | 5,500 | 11,000 | 25,000 | 47,000 | 83,000 |
| CUCUMBER ASHLEY | 1,500 | 2,500 | 4,500 | 8,000 | 17,000 | 33,500 | 63,000 |
| SQUASH BUTTERNUT | 2,000.00 | 3,500.00 | 7,000.00 | 12,000.00 | 12,500.00 | | |
| | | | | | | | |
| MBOGAMBOGA ( LEAF VEGETABLES) | | | | | | | |
| COLLARD | 1,200 | 2,000 | 3,500 | 6,500 | 13,000 | 23,000 | 47,000 |
| SPINACH F GIANT | 1,200 | 2,200 | 3,500 | 6,500 | 14,000 | 27,500 | 53,500 |
| RAPE/SARO/LOSHUU | 1,500 | 2,000 | 4,000 | 7,000 | 15,000 | 25,500 | 47,000 |
| SPIDER PLANT | 1,000 | 1,500 | 3,000 | 4,500 | 10,500 | 17,000 | 31,500 |
| KALE THOUSAND HEADED | 1,200 | 2,200 | 4,200 | 8,000 | 19,000 | 29,000 | 57,000 |
| AMARANTHUS - WHITE | 1,000 | 1,700 | 2,800 | 5,000 | 10,500 | 19,000 | 31,500 |
| AMARANTHUS - BLACK | 1,000 | 1,700 | 2,800 | 5,500 | 11,500 | 22,000 | 39,500 |
| BLACK NIGHT SHADE | 1,500 | 2,000 | 3,500 | 6,500 | 15,000 | 24,000 | 46,500 |
| VIUNGO | | | | | | | |

| AINA | 5GM | 10GM | 25GM | 50GM | 100GM | 250GM | 500GM | 1KG |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| DILL | 1,500 | 2,000 | 3,000 | 5,000 | 9,000 | 22,000 | 41,000 | 80,000 |
| FENNEL | 2,000 | 3,000 | 6,500 | 12,500 | 23,000 | 57,000 | 108,000 | 210,000 |
| BASIL | 2,000 | 3,000 | 6,500 | 12,500 | 23,000 | 57,000 | 108,000 | 210,000 |
| PARSELY | 1,500 | 2,000 | 3,000 | 5,000 | 9,000 | 22,000 | 41,000 | 80,000 |
| PEA ITALIAN | 1,500 | 2,000 | 3,000 | 5,000 | 9,000 | 22,000 | 32,000 | 57,000 |
| CORRIANDER | | 1,500 | 2,000 | 3,000 | 5,000 | 10,500 | 19,000 | 33,000 |
| BEETROOT | | 1,500 | 2,000 | 3,000 | 5,000 | 10,500 | 19,000 | 33,000 |
| LEEK ITALIAN | 2,000 | 2,500 | 4,500 | 8,000 | 15,000 | 36,000 | 70,000 | 133,000 |
| LETTUCE GREAT LAKES | | 2,000 | 3,500 | 6,500 | 11,500 | 31,000 | 56,000 | 107,000 |
| CELERY | | 2,000 | 4,000 | 6,000 | 10,500 | 25,000 | 40,000 | 68,000 |

| | 1GM | 2GM | 5GM | 10GM | 25GM | 50GM | 100GM | 250GM | 500GM | 1KG | 500SEED | 1000SEED |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MBEGU ZA CHOTARA (HYBRID) | | | | | | | | | | | | |
| KABICHI | | | | | | | | | | | | |
| GLORIA F1 | - | - | | 14,500 | 34,000 | 65,000 | - | - | - | - | | |
| PRUCTOR F1 | - | - | | 15,500 | 36,500 | 69,000 | - | - | - | - | | |
| IMANI HYBRID F1 | - | - | | 12,500 | 29,000 | 55,000 | - | - | - | - | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| HOHO (CAPSICUM) | | | | | | | | | | | | |
| VICTORY F1 | 5,000 | 9,500 | 19,500 | 38,000 | 92,000 | 180,000 | 360,000 | 880,000 | 1,740,000 | - | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| NYANYA (TOMATOES) | | | | | | | | | | | | |
| TOMATO MONIKA | 21,500 | 42,000 | 105,000 | 210,000 | 523,000 | 1,047,000 | | | | | 32,000 | 63,000 |
| TOMATO MILELE | 12,000 | 24,000 | 60,000 | 118,000 | 260,000 | 340,000 | - | - | - | - | 32,000 | 63,000 |
| TOMATO NYOTA F1 | 5,000 | 10,000 | 27,000 | 53,000 | 105,000 | 190,000 | - | - | - | - | | |
| TOMATO KIBO STAR FI | 8,000 | 16,000 | 43,000 | 85,000 | 180,000 | 350,000 | - | - | - | - | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| TIKITI MAJI (WATERMELON) | | | | | | | | | | | | |
| PRINCESS F1 | | | 2,000 | 4,500 | 9,500 | 20,000 | 36,000 | 90,000 | 180,000 | 350,000 | | |
| ZAWADI | - | - | 2,500 | 5,000 | 9,500 | 21,000 | 38,000 | 93,000 | 185,000 | 360,000 | | |
| JULIANA F1 | | | | 3,500 | 7,500 | 15,500 | 30,000 | 74,000 | 147,000 | 290,500 | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| BUTTERNUT ATLAS F1 | | | 5,500 | | | | | | | | | |
| PAPAYA USHINDI F1 | - | - | 5,500 | 21,500 | 39,500 | - | - | - | - | - | | |

**ANGALIZO**

Bei hizi zinaweza kubadilika kutokana na mwenendo wa soko, na mabadiliko fedha za kigeni kwa zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi

# Askofu Katoliki akemea ubinafsi, uvunjifu wa amani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASKOFU wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Mhashamu Isaac Amani, ameonya watu wanaochezea amani ya nchi au kuingiza ubinafsi, tofauti za kimtazamo, dini na masuala yasiyompendeza Mungu.

Badala yake, amewasihi Watanzania kila mtu kuiombea amani ya nchi, ili iendelee kuwepo kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho na kamwe isichezewe.

Akizungumza jana katika misa ya Maadhimisho ya Kilele cha Jubilei ya miaka 60 ya jimbo hilo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1963, Askofu Amani, aliwataka Watanzania kuishi kwa vitendo kauli mbiu ya jubilee hiyo ya amani na umoja vitawale.

Alisema ili kudumisha amani ni vema kila mmoja kufahamu misingi ya kulinda amani hiyo ni pamoja na kuhakikisha haki za kila mmoja hazikanyangwi, ili kila mmoja aishi kwa amani.

"Lakini naomba tuachane na roho za visasi, fitina, uongo, ibada za unafiki ambao unafanywa unafiki barabarani, nyumbani, ofisini na hivi vitu ndivyo vinavyoendelea kwa nguvu katika jamii zetu, tujifunze kusameheana pale tunapokosena, tuwe watu wa kujali haki za wengine ili amani na umoja vitawale milele na milele," alisema.

Vilevile, alisema anakerwa na lugha za udhalilishaji kwa wanandoa pale wanapotofautiana na uvunjaji wa ndoa ambao chanzo cha uzalishaji watoto wa mtaani na mateso kwao.

Kadhalika, aliagiza makanisa yote ya Katoliki kuhakikisha yanakua na ratiba za kongamano kwa waumini wake ili elimu ya kina juu ya mfundisho ya dini yatolewe.

Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongella, alisema Rais, Samia Suluhu Hassan, analishukuru kanisa hilo kwa mchango wao wa maendeleo ya wananchi bila kujali itikadi zao na serikali itaendelea kushirikiana na taasisi zote za dini katika nyanja mbalimbali.

# Waunda rasimu ya sheria ndogo kuzuia ukatili wa kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANANCHI wa Kijiji cha Kiruweni kilichoko Kata ya Mwika Kusini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wameanza rasmi mchakato wa kuunda rasimu ya sheria ndogo ya kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia, dhidi ya wanawake na watoto.

Sheria hiyo pia itasaidia kuwawajibisha wazazi na walezi watakaoshindwa kutimiza wajibu wao wa malezi kwa watoto.

Jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Richard Mawele, alisema uamuzi wa kuunda rasimu hiyo umetokana na kukithiri kwa vitendo vya ukatili kwenye eneo hilo, hasa ubakaji na ulawiti.

"Sheria tunayokuja nayo ili kukomesha ama kupunguza vitendo hivi katika kijiji chetu, itaweka adhabu kali kwa watuhumiwa. Itang'ata na haitaangalia wadhifa, umaarufu wa mtu au utajiri alionao" alisema.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa kijiji hicho, Mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), Veronica Ullomi, alisema baada ya wananchi kujengewa uwezo kwa kupatiwa elimu kuhusiana na ukatili huo, ndipo walipofikia uamuzi huo.

Alisema mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, inayohusiana na ukatili kwa wanawake, wasichana, watoto na makundi mengine ya pembezoni na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania (FEMATA), John Bina, akizungumza na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wa Mkoa wa Arusha, alipofanya ziara ya kutembelea eneo hilo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TEA kudhibiti wadudu waharibifu kwa binadamu, wanyama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UMOJA wa Wanasayansi Wanaodhibiti Wadudu Waharibifu wa Mazao nchini (TEA), umeahidi kuendelea kufanya utafiti wenye kuleta matokeo sahihi ya kukabiliana na wadudu waharibifu, ambao wanaleta athari kwa afya za binadamu, wanyama na mazingira.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Prof. Joseph Ndunguru aliyasema hayo katika mkutano mkuu wa mwaka wa wanasayansi waudhibiti wa visumbufu vya mazao unaofanyika jijini Arusha.

Alisema uwepo wa majadiliano ya utafiti, utasaidia kuongeza tija na kuboresha uzalishaji wa mifugo mazao na kuongeza soko na usalama wa chakula nchini.

"Mkutano huu ni jukwaa la kuona umuhimu wa utafiti wetu wa mazao na viuatilifu, zinapata nafasi ya kuongeza uzalishaji wenye tija sanjari na kupata uzoefu kwa wanasayansi, ili kuboresha na kuondoa matatizo ya visumbufu vya mazao," alisema.

Mwenyekiti wa TEA, Prof. Gration Rwegasira alisema mkutano huo ni jukwaa la wanasayansi kujenga mahusiano kwa kuchanganya uzoefu katika na bunifu, kwa lengo la kuboresha viuatilifu vya mazao kuleta tija ya uzalishaji.

Mwakilishi kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Deogracious Protas, alisema wataendelea kushirikiana na kuwezesha watafiti kubuni na kufanya utafiti mbalimbali kwa kutoa fedha ili kuboresha na kuongeza tija ya maendeleo ya utafiti nchini.

Alisema serikali kupitia COSTECH, imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya utafiti, ndiyo maana wameshiriki mkutano huo kwa lengo la kuendeleza utafiti wa mazao na viuatilifu sanjari na kupambana na visumbufu vya mazao.

# KKKT yachukizwa kukithiri matukio ya ukatili kwa watoto

**Na Steven William** MUHEZA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limekemea vikali kuendelea kuwepo kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto nchini.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mchungaji Kiongozi wa KKKT Usharika wa Muheza Mjini mkoani Tanga, John Ndimbo katika Sherehe ya Sikukuu ya Mikaeli na Watoto iliofanyika KKKT Mtaa wa Ngwaru.

Ndimbo alikemea kuendelea kuwepo kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto nchini, ikiwemo ubakaji, vipigo, ulawiti, utelekezaji watoto, mimba na ndoa za utotoni.

Alisema kuendelea kwa matukio hayo imekuwa ni kero kwa watoto kwani yamekuwa yakiwaathiri kisaikolojia na hata kushindwa kutimiza ndoto zao.


Hivyo, aliwaomba pia wazazi, waache tabia ya kumaliza kesi kimya kimya dhidi ya watuhumiwa wa matukio ya ukatili, hata kushindwa kwenda kutoa ushahidi mahakamani na watuhumiwa kuachiwa huru, jambo ambalo linachochea matukio hayo kuendelea kuwepo.

Katika hatua nyingine aliwataka wazazi na walezi kanisani hapo wilayani Muheza kuwalea watoto katika maadili mema na misingi ya kiroho, kuwatimizia mahitaji yao yote na kuacha kuwatelekeza.

Naye Mchungaji Msaidizi wa kanisa hilo, Yona Mgonja aliwataka wazazi kuwasimamia watoto kutimiza ndoto zao pamoja na kuwalinda dhidi ya matukio ya ukatili.

Mwinjilisti kanisa hilo, Anael Urio alikemea vitendo vya ukatili kwa watoto wadogo na kuomba serikali wanaopatikana na makosa hayo wapate adhabu kali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ibada KKKT Usharika wa Muheza Mjini mkoani Tanga, Gasper Mnken alisema kuwa watoto wa KKKT Usharika wa Muheza Mjini wamesheherekea Sikukuu ya Mikaeli na watoto kanisani hapo kula chakula, vinywaji, kupewa zawadi mbalimbali na kukemea matukio ya ukatili dhidi yao watoto.





# Wanahabari wawakutanisha wadau kupata ufumbuzi mgawo wa umeme

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAANDISHI wa habari mkoani Shinyanga wameingilia kati suala la kukatika kwa umeme linaloendelea nchini kwa kuwaweka pamoja wadau wa nishati ili kupata mawazo mbadala juu ya suluhu ya suala hilo.

Wadau hao waliokutanishwa juzi katika mdahalo ni pamoja na watumiaji wa nishati ya umeme ambao ni wafanyabiashara, mafundi wa fani mbalimbali na maofisa kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Shinyanga.

Katika mjadala huo wadau hao waliishauri serikali kupitia Wizara ya Nishati kuweka nguvu zaidi katika vyanzo vingine vya uzalishaji umeme ikiwa ni pamoja na mfumo wa jua, upepo, joto ardhi pamoja na gesi na siyo kutegemea maji kwa asilimia kubwa.

Mmoja wa wadau hao, Nassoro Warioba, alisema kuwa licha ya serikali kuanzisha vyanzo mbalimbali vya umeme uendelezwaji wake umekuwa mdogo hali inayosababisha kuwa tegemezi zaidi katika kimoja ambacho ni maji.

"Kukatika kwa umeme licha ya kupewa taarifa zinazokinzana kunaweza kuwa kunasababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi kwani kwa sasa mvua ni chache hivyo nguvu ya chanzo hicho ni ndogo, lakini kwa muda huu jua lipo la kutosha mifumo ya umeme jua ingelikuwa suluhisho kwa sasa,"alieleza.

Naye Dk. Kulwa Meshaki, alieleza kuwa serikali inapaswa kuruhusu kampuni binafsi kuwekeza katika sekta hiyo ili kuwepo kwa ushindani baina yao na TANESCO hali ambayo itasaidia tatizo la umeme nchini kubaki kuwa historia.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Shinyanga, Jonathani Manyama, alisema tatizo la kukatika kwa umeme limeathiri shughuli nyingi za kiuchumi na hata wawekezaji wameanza kuogopa kuja kuwekeza nchini kwani hakuna umeme wa uhakika.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Shinyanga, Mhandisi Elias Tunrbull, alisema tatizo la kukatika kwa umeme linatokana na vyanzo vya uzalishaji umeme kupungukiwa maji, huku matumizi ya umeme yakiwa ni makubwa.

Alisema matumizi ya umeme kwa nchi nzima kwa sasa ni megawatts 1,482.8 lakini uzalishaji upo chini ya megawatts 1,000 na kwamba vyanzo vyote vya uzalishaji umeme vingekuwa vinafanya kazi, umeme ungezalishwa Megawatts 1,570 na kusingekuwapo na kero ya kukatika kwa umeme.

Alisema serikali imeendelea kuchukua hatua ya kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme ikiwamo na ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo litakuwa likizalisha umeme megawatts 2,115 na tatizo la kukatika kwa umeme litabaki kuwa historia na hakutakuwa na mgawo tena.

Aidha, alisema pia serikali imeendelea kuibua vyanzo vingine vya uzalishaji umeme, ikiwamo umeme wa jua ambao unatekelezwa wilayani Kishapu megawatts 150 na kwamba katika Mkoa wa Shinyanga mradi huo ukikamilika hakutakuwa na tatizo la umeme mkoani hapa.




Wafanyakazi wa Benki ya Azania wakiongozwa na Meneja wa tawi la Geita, Rhoda Baluhya (wa pili kushoto), wakifurahia baada ya kuibuka washindi wa kwanza kwa taasisi za kifedha katika Maonyesho ya 6 ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini mkoani Geita yaliyotamatika Jumamosi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM Tarime yapitisha taarifa ya MUWASA waliyoikataa awali

**Na Timiothy Itembe,**
TARIME

KIKAO cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tarime kimepitisha taarifa ya utekelezaji wa kazi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) Kanda ya Tarime.

Kikao hicho pia kimejadili mpango wa utekelezaji wa MUWASA baada ya hapo awali kuikataa taarifa hiyo.

Akiongea katika kikao hicho juzi Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Tarime, Daud Ngicho aliwaambia wajumbe kuwa hapo awali walifuata mkumbo wa watu wa Bunda kwa kukataa taarifa hiyo, lakini baada ya kufuatilia na kuridhika na utendaji kazi wake imebidi waipokee na kuipitisha.

Hivyo, aliwaomba wajumbe wa kikao hicho kupokea taarifa hiyo ya MUWASA kwani imejikita katika utekelezaji wa sera na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2020-2025 na kwamba kutoipokea ni kukwamisha shughuli za maendeleo kwa jamii.

"Tunatakiwa sasa kujadili utekelezaji wake na pale tutakapoona kuna makosa tukosoe kwa lengo la kuhakikisha tunajenga na kuboresha utendaji kazi wa mamlaka hii ili ifikishe huduma kwa wananchi kama ilivyo katika malengo ya ilani yetu,"alisema Ngicho.

Katibu wa chama hicho wilaya, Noverty Kibaji alisema kukataa taarifa hiyo siyo suluhisho la kumaliza kero za upatikanaji wa maji kwa wananchi na kinachotakiwa ni kushughulika na mapungufu ya utekelezaji ili yafanyiwe kazi.

Akiwasisilisha taarifa ya mamlaka hiyo Kanda ya Tarime kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa MUWASA, Mkurugenziwa Huduma kwa Wateja, Edward Range alisema kuwa wametekeleza mpango wa muda mfupi kwa kupeleka maji Shule ya Sekondari Tarime.

Vilevile, alieleza kuwa mamlaka hiyo imenunua gari kwa ajili ya utoaji wa huduma na kuwafikia wananchi kwa wakati.

Alisema kuwa mradi huo unagharimu Sh.bilioni 134.399 na unategemea kukamilika ifikapo Julai 23, 2025 ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia nane.

# Hiki hapa chanzo vikundi vya wajasiriamali wanawake kufa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa elimu ya fedha kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali wilayani Kahama mkoani Shinyanga umetajwa kuwa sababu ya vikundi hivyo kufa, huku washiriki wakitokomea na kuziacha familia zao kwa kushindwa kurejesha mikopo hiyo.

Pia, wajasiriamali hao wanachukua mikopo ambayo hawawezi kumudu urejeshwaji wake, hivyo kuhitaji suala hilo kuwa miongoni vya vipaumbele katika utolewaji wa elimu ya watu wazima ili kuwasaidia katika kujiinua kiuchumi.

Mmoja wa wajasiriamali hao Asha Hussein kutoka Kikundi cha ujasiriamali cha Jitambue Mtaa wa Nyakato, Kata ya Nyasubi alisema kuwa idadi kubwa ya wanawake wajasiriamali wanajiingiza kwenye mikopo umiza bila kujua hali inayosababisha wanafirisika badala ya kukua kimtaji.

Asha ambaye ni mwalimu wa usajasiriamali wilayani hapa aliongeza kuwa, ili kuondoa adha hiyo ni vema elimu ya ujasiriamali inafundishwa shuleni ili wanafunzi wanaokosa nafasi ya kuendelea kimasomo wajiajiri.

"Tunafundishwa juu ya kutafuta pesa na si kutumia pesa kama inavyotakiwa, hivyo kama elimu ya ujasiriamali itatolewa vizuri shuleni tunaweza tukawa na taifa lenye wataalumu wengi na kuweza kutambua fursa za ajira na siyo kutegemea ajira kutoka serikalini kama ilivyozoeleka," alisema.

Ofisa Elimu Taaluma Sekondari, Stephen Ngemela alisema, elimu ya watu wazima nje ya mfumo rasmi inahusisha shule za sekondari na msingi na katika Manispaa ya Kahama kuna wanafunzi 431 wanasoma Mpango wa Elimu Maalum kwa Watu Wazima (MEMKWA) na wamekuwa wakifanya vema kila mwaka.

Aidha alisema, kuna vikundi 25 ambavyo vinajifunza ujasiriamali, vituo vinne vya ufundi stadi kati ya hivyo viwili viko chini ya Halmashauri ya Manispaa na kusema kikwazo kikubwa katika maendeleo ya elimu hiyo kuwa ni upungufu wa walimu na imani potofu.




Samia, viongozi wanawake ni kioo jamii kuacha ukatili kijinsia




Unyanyapaa waraibu unavyowapokonya haki za ajira, urithi, huduma za jamii

Nipashe
TESA
Jumanne Oktoba 3, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Mafuta, gesi, makaa ya mawe vinaangamiza dunia

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Wakati mgawo ukitikisa, mbunifu aja na mbadala

• Awasha mtambo kuzalisha umeme kwa maji ya kisima

GEORGE Rubagumya maarufu Bwemelo, anaweza kuitwa mbobezi wa sayansi, ambaye licha ya kwamba haoni, anafanya maajabu kwenye ubunifu na sasa anaufanyia majaribio mtambo wa kufua umeme wa maji ya kisima.

Mkazi huyo wa Segerea Dar es Salaam, anasema umeme wake ni nishati ya kudumu isiyotegemea maji ya mito, ambayo wakati wa kiangazi yanakauka kama ilivyo Mtera na Kidatu na kusababisha TANESCO kutangaza mgawo.

Anaiambia Nipashe kuwa mtambo huo utazalisha wati 42,000 za umeme kutoka kwenye kisima kinachochimbwa mahali popote kulingana na mahitaji ya mteja.

"Ni kama kusema teknolojia hii inatengeneza maporomoko ya maji sawasawa na yale yanayotumika kwenye mabwawa, haihitaji mto kujaa maji, mvua kunyesha wala upepo. Iwe kiangazi, kipupwe umeme wake ni wa kutosha ukishajaza maji umepata nishati," anasema.

" Chanzo hiki kinaweza kuwa mbadala wa vyanzo vyote vya umeme jadifu nchini," anasema na kusisitiza kuwa: " Tunaweza kupata hata umeme mwingi kama wa TANESCO endapo tutatengeneza kisima kikubwa kwa teknolojia hii."



Bwawa la kufua umeme Mtera ni chanzo kinachotishiwa na ukame na kusababisha mgao. **PICHA: MTANDAO**

Anataja faida za mradi wake kuwa ni kupata umeme wa uhakika wakati wote kwa bei nafuu na mahali popote na kwamba mtambo huo unaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji mashamba, taasisi kubwa zikiwamo shule na hospitali.

"Hiki ni chanzo cha kuaminika cha umeme tofauti na vingine ambavyo ni vya kubadilika kulingana na hali ya hewa na upatikanaji wa mvua kwa sababu maporomoko yake ya maji ni ya asili, lakini mtambo huu unatengeneza mwenyewe," anasema.

Maporomoko hayo ya maji yanasaidia kuvuna umeme huo kwa jenereta kama injini katika mradi huo ambayo haitumii mafuta kama ilivyozoeleka, anasema.

"Teknolojia hii haina cha kubadilika kwa sababu maji yanazunguka hapo tangu mwanzo wa mwaka hadi mwisho wa mwaka. Popote unaweza kuweka iwe jangwani, bondeni, kwenye mwinuko na baharini ni wewe tu," anasema mtaalamu huyo.

**MAJARIBIO**

Anasema ameanza kuufanyia majaribio maeneo ya Segerea na ameupa jina la injini ya Tanzanite.

Aidha, anasema umeme huo unaweza kutumiwa na wateja kati ya nyumba 10 hadi 25 ambazo matumizi yake ni ya kawaida.

Bwemelo, anasema alianza kujenga mtambo huo, Julai mwaka jana na baada ya majaribio ya awamu ya kwanza alipata mafanikio.

"Imenipa imani ya kuendelea na hatua zilizobaki za kukamilisha ujenzi wa mradi wangu... Ni hatua kubwa na nina kila sababu ya kujisifu na kujivunia kwani mafanikio makubwa kwangu yatakayoleta tija kwa taifa na faida kwa jamii," anasema, Bwemelo ambaye ni mwalimu wa sayansi.

Anakumbusha kuwa utafiti wa mradi huo alianza 2018 kwa lengo la kupata suluhisho la tatizo la mgawo wa umeme nchini kutokana na sababu mbalimbali.

Anasema endapo ujenzi wa mradi huo utakamilika, anaamini utapunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya umeme na kwa wateja watakaohitaji kupelekewa huduma hiyo.

Anasema teknolojia hiyo inatumia mabomba maalum kutoka kisimani ambacho kimechimbwa karibu, kusukuma maji kwenda juu kwa nguvu kubwa na kurudi kwenye kisima hicho, kisha kuzalisha umeme huo jadilifu.

Bwemelo anasema maji hayo yanaweza kutumika kuendelea kuzalisha umeme kwa zaidi ya mwaka yakiwa yanazunguka ndani humo. Mwalimu huyo wa masomo ya sayansi na hisabati, anasema ujenzi wa mradi huo unafanyika kwa kusuasua kutokana na kukosa fedha za kununua vifaa.

Kadhalika, anasema hadi sasa ametumia Shilingi 6,000,000, kati ya milioni 14 zinazohitajika kukamilisha ujenzi wa mradi huo.

Anaonyesha hofu kuwa gharama zinaweza kuongezeka kutokana na bei za vifaa kupanda kila wakati kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo bei ya mafuta kuongezeka.

Anasema umeme wake huo unaweza kutumika ofisini, viwandani, hospitalini na wateja mitaani.

Kwa mujibu wa Bwemelo, mtambo huo ni rahisi kwa sababu hautumii nguzo nyingi, nyaya, transfoma na vifaa vingine ambavyo vingegharimu fedha nyingi. Anaeleza kuwa umeme unaweza kuzalishwa kwa kiwango chochote kulingana na uwekezaji na si vinginevyo.

Anazungumzia nchi zenye mito michache tofauti na Tanzania lakini zina umeme wa kutosha kulingana na mahitaji yake na vyanzo mbadala.

INAENDELEA UK.12

ELIMU NA TUNTULE SWEBE

# Rais Samia, viongozi wanawake ni kioo jamii kuacha ukatili kijinsia

KILA mwaka Oktoba 11 ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Duniani. Ndiyo wakati wa kuangalia, kuibua na kushughulikia matatizo, mahitaji na changamoto zinazowakabili mabinti.

Yote hayo yanafanyika kuwezesha wasichana kupata haki zao za kibinadamu na maisha bora bila kubaguliwa au kutengwa.

Wakati siku hiyo ikikaribia, jamii nyingi za Tanzania japo kwa kiasi zinaonekana kuwa na mtazamo hasi kwa watoto wa kike. Ndiyo maana wanaelezwa kuwa wapo wanaume wanaowatelekeza wake zao, kisa wanazaa wasichana.

Chuki dhidi ya wasichana zinasababisha kuwatesa na kuwanyanyasa wazazi ambao hawakujaliwa kuzaa watoto wa kiume. Kuna baadhi ya kinamama wanadai kuwa baada ya kujifungua waume zao huwatusi badala ya kuwapa pole na hongera ya kupata mtoto.

Katika mahojiano na baadhi ya kinamama kwenye wodi za wazazi jijini Mbeya, wanasema kama ukipata watoto wa kike pekee kwenye familia unapokea kejeli na mizaha.

Mfano, kuna wanaume wanaowaambia wake zao, tutafungua chuo kikuu cha wasichana hapa nyumbani. Wengine wanawasalimia wenza wao kwa kejeli mfano hujambo 'wewe na mabaa medi wako?'

Kuwadharau wasichana na watoto wa kike kumesabisha kuendeleza hata leo mila na desturi zinazoumiza watoto wa kike kama mimba na ndoa za utotoni, ukeketaji na matendo ya ukatili dhidi



Rais Samia Suluhu Hassan akionyesha mapenzi kwa watoto. **PICHA: MTANDAO**

yao kama ubakaji, kutumikishwa kama 'hausi geli' na unyanyasaji wa aina mbalimbali.

Kwa mfano ipo mikoa mashuhuri kwa ndoa za utotoni kama Shinyanga, ambayo Takwimu za Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) linautaja ukiongoza kwa asilimia 59, mwingine ni Tabora wenye asilimia 58, Mara 55, Dodoma 51 na Lindi wenye asilimia 48.

UNICEF inasema sababu kuu zinazochangia kukua kwa tatizo hilo ni pamoja mila na desturi potofu, uwepo wa sheria na sera zinazopingana, uongozi katika ngazi ya kata, vijiji, mitaa na vitongoji kushindwa kukabiliana na tatizo hilo.

Licha ya ndoa za utotoni mabinti wa taifa hili pia wanatumika kufanya kazi za nyumbani kwa ujira mdogo, ambako nako wananyanyaswa na kudhalilishwa na wale waliowaajiri ambao wengi ni wanawake.

Licha ya juhudi nyingi kufanyika zipo familia, jamii na hata wasichana wanaoamini kuwa watoto wa kike (wanawake) hawana haja ya kusoma na kuendelea kitaaluma.

Wanaendeleza mifumo ya kuwa na fikra kuwa wasichana lao ni kuolewa na kuwatumikia wanaume hali inayoendeleza ndoa, mimba utotoni na kuwaajiri kama watumishi wa ndani.

Kuna baadhi ya misemo inayosisitiza kuwapa kipaumbele wanawake kwa mfano, ukimwelimisha mtoto wa kike umelisomesha taifa. Kadhalika, upo usemao hakuna nguzo kuu ya uthabiti kuliko mwanamke mwenye nguvu, uhuru, na mwenye elimu. Huyu ndiye mwenye ufahamu.

Upo mwingine kuwa ikiwa watu watataka kuona maendeleo endelevu duniani, uwekezaji bora ni kwenye kuwaendeleza wanawake hasa kwenye elimu.

Wanawake kukosa elimu na kuendelea kuchukuliwa kama watu duni kumesababisha watoto wa kike kutokujiamini.

Hali hii imedumaza mitazamo yao na kusababisha kuvunjika moyo na kuendelea kubakia kuwa watu wasiojiamini na wasioaminika .

Athari mojawapo za kushindwa kujiamini zinaonekana kwenye ajira.Wengi wanatumikishwa bure. Hawalipwi wala hawawezi kudai mishahara yao ,

Wapo waajiri ambao ni kinamama anamwambia binti nakutunzia mshahara wako kwa kila mwezi lakini pia hamlipi hata mwaka unamalizika na wanashindwa kudai wengi wakiishia kufanyakazi hata miaka mitano na kuondoka bila malipo.

Baadhi ya mikoa inayoendeleza kunyanyasa wasichana na kuwanyima haki ya elimu, ingetarajiwa kuanzia sasa iamke kwa kuona kinamama vielelezo mfano Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Na zaidi Rais Mama Samia Suluhu Hassan.

Viongozi hawa wawe hamasa kwa mabinti na wanafunzi wa kike wa Tanzania wakifahamu kuwa nao pia walikuwa watoto wa kike waliolelewa na jamii na wazazi, walezi ambao pia walikuwa kwenye taifa lenye mila za kutowapa wanawake kipaumbele.

Lakini, wamesoma na mpaka sasa ni watu walioacha historia kwenye maendeleo ya Tanzania.

Jamii inatakiwa kuongeza hamasa na kuhimiza wasichana na mabinti kuwa na uthubutu na kuwajengea imani kuwa juhudi za kielimu ndizo zitafanikisha kupata matunda bora.

Uwepo wa viongozi wengi wakuu wanawake uwe ni mwanzo wa kuachana na mila potofu,wanajamii kuamka na kuwa na mtazamo chanya kwa watoto wa kike, kwani ikiwatetea kuwalinda na kuwainua kielimu ndiko kuwa na mama bora wa baadaye.

Jamii hasa za mikoa inayokumbatia mila kandamizi zianze kumpa haki ya msingi mtoto wa kike, kwa kuwa ndiye mtunza jamii ajaye.

# Wakati mgawo ukitikisa, mbunifu aja na mbadala

**INATOKA UK.11**

Anazungumzia nchi zenye mito michache tofauti na Tanzania lakini zina umeme wa kutosha kulingana na mahitaji yake na vyanzo mbadala.

Bwemelo anakisia kuwa umeme duniani hauzidi megawati 5,000,000 lakini kwa teknolojia yake anaweza kuzalisha zaidi ya huo endapo atapata fedha za uwekezaji mkubwa.

**FAIDA KIUWEKEZAJI**

Akizungumzia faida ya umeme huo, anasema upatikana kwa bei nafuu na kuachana na matumizi ya mkaa na kuni, hivyo kunusuru mazingira kutokana na ukataji miti ovyo.

Anasema kwa kuwa umeme utazalishwa kwa kiwango kikubwa na kuuzwa kwa bei nafuu kwa wateja wataondokana na matumizi ya kuni na mkaa vinavyotishia mazingira.

"Kama bei itakuwa nafuu, Watanzania wataanza kutumia umeme na kuacha kupikia kuni na mkaa na kuanza kutumia umeme huo kwani wanaweza kuuziwa kwa Sh. 50 kwa uniti moja na kununua wa Sh. 300 ambao anaweza kupikia kwa saa sita. Sasa kama bei itakuwa rahisi, mtu atakwenda kununua mkaa unaouzwa kipimo kwa Sh. 1,000?" Anahoji.

"Mabadiliko ya tabianchi yanaletwa na ukataji miti ovyo, ongezeko la joto duniani, uzalishaji wa gesi ya ukaa na matumizi ya nishati isiyo safi kama makaa ya mawe, mafuta mazito na kuni."

Anaongeza kuwa yote hayo yanasababisha joto duniani na mabadiliko mengine hatarishi kama kimbunga, mafuriko na joto kali.

Anazitaja taasisi za umma kama Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO) na Wizara ya Nishati kuwa zinaufahamu utafiti wake.

Aidha, amewahi kuwasiliana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuhusu ubunifu wa mradi huo, wataalamu wake wakamshauri awasiliane na taasisi zinazotambuliwa ili ziwapeleke ubunifu wake COSTECH.

Anawaomba wadau wa ndani na nje kumsaidia kukamilisha ujenzi wa mradi huo ili uzalishaji wa umeme uanze mara moja.

Vilevile, anaiomba Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Kazi, Vijana na Walemavu kumsaidia fedha ili akamilishe mradi huo kwa manufaa ya taifa.

**Anaomba watakaokuwa tayari wawasiliane naye kupitia Mhariri wa Nipashe au wampigie mwenyewe kwa namba 0747363813.**

ELIMU
NA GWAMAKA ALIPIPI

# Unyanyapaa waraibu unavyowapokonya haki za ajira, urithi, huduma za jamii

MATUMIZI ya dawa za kulevya yanaathiri taifa lakini zaidi vijana, yanawaharibu kimwili, kihisia na kiuchumi hivyo Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), inapaza sauti kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu athari za dawa hizo.

Ripoti ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2022 inayotolewa na DCEA, inaeleza athari nyingi za dawa hizo, ikizitaja kuwa ni chanzo cha vifo vya ghafla kwa wanaojidunga, pale wanapotumia kiasi kikubwa cha dawa (overdose).

Aidha, zinasababisha saratani, upungufu wa nguvu za kiume, kukosa usingizi, hamu ya kula na kuoza meno pia, husababisha ulemavu na upungufu wa kinga ya mwili.

Vilevile, inaeleza kuwa dawa za kulevya kwa wanawake huvuruga mtiriko wa hedhi, kuharibu mimba,kuzaliwa watoto njiti hata wenye uraibu wa dawa za kulevya, waliodumaa mwili na kiakili, wenye matatizo ya moyo na ulemavu wa viungo.

Ripoti hiyo pia inaeleza kuwa waraibu husababisha kukithiri uhalifu ikiwemo wizi, ukahaba, utapeli na uporaji ili kupata fedha za kununulia dawa hizo.

Ripoti ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2022 inataja huvuruga uhusiano, kutengana kwa wazazi, kutelekeza familia na watoto kukosa malezi bora na kukimbilia mitaani kuwa ni moja ya athari za dawa hizo.

Kadhalika inasema huchangia ongezeko la maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji walioambukizwa maradhi hayo.

Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoweza kuepukika zinazosababisha ulemavu, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu

Ripoti ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2022inagusia athari kiuchumi kuwa ni kupunguza ufanisi kazini na kusababisha kupoteza ajira au kufilisika, mtumiaji kutoajirika, umaskini, vijana kushindwa kufanya uzalishaji mali na hupoteza nguvu kazi huku taifa likigharamia fedha nyingi kutiba na kutoa elimu kwa waraibu.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa wanaojidunga dawa za kulevya husababisha uchafuzi wa mazingira kwa kutupa sindano ambazo ni hatari pia vichochoroni, viwanja vya michezo, fukweni na vituo vya mabasi.



Sindano zinazotumiwa na waraibu wanaojidunga husambaza maradhi na taka mitaani. **PICHA: MTANDAO**

**UNYANYAPAA**

Waraibu kunyanyapaliwa na familia na jamii na kusababisha wakose haki hata wanapoacha kuzitumia.Mfano, urithi, ajira na kusingiziwa uhalifu. Unyanyapaa husababisha wasijithamini na kuwa na hofu kushiriki shughuli na huduma za kijamii wakishindwa kupata tiba kwenye vituo vya afya.

Ripoti inasema unyanyapaa huwatumbukiza tena walioacha kutumia dawa za kulevya kwenye makundi ya wenzao kutafuta faraja, hivyo wakirudi tena kwenye dawa hizo

**UDHIBITI**

Kamishna wa Kinga na Tiba DCEA, Dk. Peter Mfisi, anasema kikubwa ni kutoa elimu kuelimisha na kuihamasisha jamii kuziepuka na kwamba ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi, mamlaka iliandaa mwongozo wa kutoa elimu ya dawa za kulevya.

Mfisi anasema DCEA inashirikiana na TAKUKURU kutumia klabu za wanafunzi wa msingi na sekondari kutoa elimu kwa sababu watumiaji wengi wanaanza na miaka 17 hadi 18 na wakifika ukubwani wanakuwa wameharibikiwa.

Aidha, anasema hadi sasa kuna vituo 15 vya kutolea tiba vilivyoko Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Songwe, Dodoma, Mwanza, Tanga na Arusha.

Halikadhalika mamlaka hiyo imetoa elimu kwa watumishi na wanavyuo 3,000 kutoka vyuo vya Elimu ya Biashara (CBE Dar), Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo cha Wakala wa Maendeleo ya Elimu (ADEM), Pwani na cha Mipango Dodoma, anasema.

Anaeleza kuwa DCEA inatumia vyombo vya habari kufikisha elimu ya tatizo la dawa za kulevya kwa umma, kupitia redio, runinga, magazeti, vipeperushi, majarida, mitandao ya kijamii na tovuti ya mamlaka, ikifikia wanahabari katika redio 12 za kijamii wa Lindi na Mtwara.

"Wasikilizaji wa kanda hiyo iliyokithiri kwa usafirishaji mkubwa wa dawa za kulevya walisikia ujumbe wa madhara ya dawa hizo na kuhamasishwa kushirikiana na serikali kuzidhibiti," anasema.

Anataja jarida liitwalo 'Dawa za Kulevya' linalotoa habari za mapambano ya kuzikabili linalosambazwa kwa jamii ili kuongeza uelewa, pia elimu iliwafikia maofisa maendeleo jamii na ustawi wa jamii, makatibu muhtasi, wakaguzi wa ndani wa mahesabu na wafamasia.

> Wasikilizaji wa kanda hiyo iliyokithiri kwa usafirishaji mkubwa wa dawa za kulevya walisikia ujumbe wa madhara ya dawa hizo na kuhamasishwa kushirikiana na serikali kuzidhibiti.

**VYOMBO VYA ULINZI**

Dokta Mfusi, anasema vyombo vya ulinzi na usalama vimepatiwa elimu sahihi kuviongezea ujuzi kudhibiti dawa za kulevya na maofisa 67 wa majeshi kutoka mataifa 16 ya Afrika wamehusika.

Anasema mamlaka pia ilifanya uhamasishaji wa mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa Kamati za Ulinzi na Usalama pamoja na viongozi wa kijamii wa mikoa ya Arusha, Mbeya na Mwanza.

"Katika uhamasishaji huo takribani watu 400 wamenufaika na elimu hiyo. Mamlaka ilitoa elimu kuhusu Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa maafisa upepelezi wa Jeshi la Polisi wanaoshughulikia mashauri ya dawa za kulevya mkoani Tanga," anasema.

Dk. Mfisi anasema washiriki 91 kutoka asasi za kiraia zinazowahudumia waraibu wa dawa za kulevya walipata elimu juu ya mabadiliko mbalimbali yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya ya Mwaka 2015.

**VIONGOZI WA DINI**

Vilevile anasema elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa Kamati ya Taifa ya Amani na Maridhiano inayohusisha viongozi wa dini mbalimbali. Lengo ni kufikisha elimu ya dawa za kulevya kwa waumini kwenye mahubiri yao.

Anasema mamlaka kwa kushirikiana na wadau ilitumia Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya Duniani iliyofanyika Dar es Salaam kutoa elimu na kuikumbusha jamii kuhusu tatizo la dawa za kulevya.

Aidha, anasema mamlaka ilishiriki katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa kutoa elimu ya dawa za kulevya kama vile Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) mkoani Dar es salaam, ya Siku ya Wakulima (Nanenane) mkoani Mbeya na ya Wiki ya Vijana yaliyoambatana na Kilele cha Mbio za Mwenge na Siku ya Kumbukizi ya Kifo cha Baba wa Taifa Julius Nyerere mkoani Kagera na Maadhimisho ya Wiki ya UKIMWI Duniani mkoani Lindi.

Anasema wasimamizi wa kemikali, wasafirishaji, watumiaji, wajasiriamali na walimu wa sekondari wa somo la kemia 1,669 kutoka Dar, Mwanza na Dodoma wamefunzwa kuhusu udhibiti wa kemikali bashirifu na sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ya mwaka 2015.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# Mafuta, gesi na makaa ya mawe vinaangamiza dunia

• Kuelekea mwisho wa enzi hakuna nishati salama



Kituo cha kufua umeme wa gesi cha Kinyerezi 11 jijini Dar es Salaam, gesi asilia inaelezwa kuwa chanzo cha ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: TANESCO**

KUELEKEA mkutano wa mazingira wa COP28 Umoja wa Mataifa (UN) unasema bado mataifa hayajafanikiwa kudhibiti nishati ya visukuku inayohusisha gesi, mafuta na makaa ya mawe ambayo inaongeza joto kuanzia ardhini, baharini, angani na anga za juu na kuukaribisha mwisho wa dunia .

Mkutano wa kilele wa mazingira wa Umoja wa Mataifa wa COP 28 unatarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu ikiwa imebakia miezi miwili kufikia siku hiyo, bado dunia iko nyuma na haijapata muafaka wa kuziba pengo baina ya wale wanaodai mpango wa kuachana na nishati za visukuku zinazoongeza joto duniani na mataifa yanayosisitiza kuendelea na matumizi nishati hizo.

Mkutano wa COP28 utakaofanyika Dubai kuanzia Novemba 30 na Desemba 12 unaonekana kama fursa muhimu kwa serikali za mataifa duniani kuharakisha hatua za kupunguza ongezeko la matumizi ya nishati za visukuku, lakini bado kuna mgawanyiko mkubwa juu ya siku zijazo katika

> "Umoja wa Ulaya na mataifa mengine yanayopigania nishati salama kwa mazingira wanasema ni muhimu kuongoza kwa sera na uwekezaji uliojitenga mbali na nishati zinazochafua hali ya hewa.

athari ya nisti hizo.

Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwishoni mwa mwezi uliopita uliibua tena mjadala wa muda mrefu huku mataifa yanayokabiliwa na athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi, kama vile Visiwa vya Marshall, yakiziomba nchi tajiri kuachana na nishati zinazochafua mazingira na kuwekeza katika njia mbadala.

Akizungumza katika mkutano wa kilele wa tabianchi uliofanyika sambamba na mkutano ule wa baraza kuu, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, anasema "binadamu wamefungua milango ya kuzimu." Akimaanisha wanajiangamiza.

Kauli hiyo ikitafsiriwa na wanamazingira kwamba alikosoa ulafi wa watu walio na maslahi katika matumizi ya nishati za visukuku. Nchi nyingine zinazotoa au kutegemea visukuku zimesisitiza uwezekano wa matumizi ya teknolojia ili "kupunguza" uchafuzi, lakini wakiwa na maana ya kudhibiti tu utoaji wa nisahti hizo, badala ya kukomesha kabisa matumizi yake.

China haijaonesha nia ya kuachana na visukuku na ndilo taifa mtumiaji mkubwa zaidi wa nishati za visukuku duniani tena ni miongoni mwa nchi zinazoashiria kwamba zitaendelea kutumia kwa miongo kadhaa.

Marekani inasema inasisitiza kuunga mkono hatua ya kuachana na visukuku huku ikikubali kwamba kuna mipango ya baadhi ya nchi zinazoendelea kuwekeza katika nishati hizo. Ingawa mjumbe wa mabadiliko ya tabianchi wa Marekani, John Kerry, anahoji ikiwa teknolojia ya kudhibiti utoaji wa hewa chafu inaweza kupatikana kwa haraka.

Umoja wa Ulaya na mataifa mengine yanayopigania nishati salama kwa mazingira wanasema ni muhimu kuongoza kwa sera na uwekezaji uliojitenga mbali na nishati zinazochafua hali ya hewa.

Aprili mwaka huu, kundi la mataifa ya G7 ambazo ni pamoja na Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan, Uingereza, Marekani na Umoja wa Ulaya, ziliahidi kuachana mara moja na matumizi ya mafuta ya kisukuku na kuyataka mataifa mengine kufuata mkondo huo. Aidha, pamoja na kutangaza hatua hiyo, kundi hilo lilishindwa kukubaliana juu ya ukomo au mwisho wa matumizi ya vyanzo vya nishati vinavyochafua hali ya hewa, kama makaa ya mawe na mafuta ya petroli.

Hatua hiyo inaashiria mgawanyiko mkubwa miongoni mwa washirika unaolenga kuleta usawa kati ya mabadiliko ya tabianchi na usalama wa nishati.

Lakini kwa kuzingatia mgawanyiko uliopo juu ya mustakabali wa nishati za visukuku, huku zaidi ya nchi 80 zikijaribu bila mafanikio kufikia makubaliano katika mkutano wa kilele wa COP27 mwaka jana. Na kinachoendelea sasa wanatafuta misamiati mipya katika kutafuta maelewano.

Katika kile kilichoonekana kama mafanikio yanayowezekana mnamo Aprili, kundi la mataifa saba yaliyoendelea kiviwanda duniani, G7 lilikubali kuharakisha kile walichokitaja kuwa ni mchakato wa kuondoa mafuta yasiyobadilishwa.

Kwa kutumia msamiati wa "yasiyobadilishwa", ahadi hii ililenga mafuta yaliyotumika bila ya kutumia teknolojia ya kupunguza hewa chafu. Lakini kufikia Julai, ahadi hiyo iliyumba wakati kundi la G20 ambalo linajumuisha watowaji wa mafuta na gesi kama Saudi Arabia na Urusi liliposhindwa kufikia muafaka juu ya suala hilo.

**WANAKWAMA WAPI?**

Mkwamo uko wapi kuondoa nishati ya visukuku? Pengine ni swali wanalojiuliza wengi, Waziri wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Ireland, Eamon Ryan, anasema suala la kuondoa mafuta yote ya visukuku au utengenezaji wake linaweza kuwa gumu zaidi katika mkutano wa COP28.

Kundi la nchi 17 - zikiwemo Ufaransa, Kenya, Chile, Colombia na mataifa ya visiwa vya Pasifiki va Tuvalu na Vanuatu , wiki iliyopita lilitoa wito wa kuondolewa kwa mafuta ambayo yanazuia matumizi ya teknolojia ya kuondosha hewa chafu kwenye tabaka la hewa la ozoni.

Makampuni yanayozalisha mafuta na gesi yanasema dunia itahitaji teknolojia ya kupunguza uchafuzi ili kuwezesha uzalishaji zaidi wa nishati wenye uchafuzi unaohimilika. Lakini baadhi ya nchi zinazoendelea pia zinazopinga kuondolewa kwa nishati za visukuku zinasema zinahitaji nishati hiyo ili kuongeza uzalishaji wa umeme katika kuboresha maendeleo ya kiuchumi kwa njia sawa kama Japan na Marekani.

Ndani ya Umoja wa Afrika (AU), baadhi ya serikali zimeshutumu nchi za Magharibi kwa unafiki kwa kutumia hoja za kuhifadhi hali ya hewa lakini zikikataa kufadhili miradi ya gesi katika mataifa yanayoendelea, wakati mataifa hayo yakiendelea kuchoma gesi kwenye nchi zao. **DW**



## Vifo vya mama na mtoto mkoani Dodoma vyapungua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu amesema Utafiti wa Hali ya Afya wa mwaka 2022 unaonyesha viashiria vya huduma ya afya ya uzazi kwa mkoa wa Dodoma inafanya vizuri, kutokana na vifo vya mama na mtoto kupungua siku hadi siku.

Gugu aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa utekelezaji wa mradi wa afya ya mama na mtoto uliofanyika jijini hapa.

Alisema hatua hiyo imekuja na idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya afya kwa Mkoa wa Dodoma kuwa chachu ya utoaji wa huduma bora za afya.

"Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Mkoa wa Dodoma una vituo vya afya 542 ikiwa ni pamoja na hospitali 16, vituo vya afya 69, zahanati 436, hivi husaidia sana katika utoaji huduma,"alisema Gugu.

Alibainisha idara ya afya chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma imefanya tathmini ya utekelezaji wa mradi huo wa huduma ya afya ya uzazi na mtoto ambao unatekekezwa katika Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa.

Aliishukuru taasisi ya nchini Korea inayojulikana kama Korea Foundation For International Health Care (KOFIH) kwa kudhamini mradi huo ambao umeleta matokeo chanya.

Alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Mkoa wa Dodoma una vituo vya afya 542 ikiwa ni pamoja na hospitali 16, vituo vya afya 69, zahanati 436 na kliniki maalum 21.

Aidha, katika taarifa iliyotolewa na Mratibu wa Huduma za afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Dodoma, Nice Moshi inaonyesha kuwa KOFIH imetekeleza mradi wa miaka mitano wa huduma ya afya ya uzazi na mtoto kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Alisema katika kipindi hiki cha miaka miwili, Halmashauri ya Kongwa na Mpwapwa zimenufaika na uboreshwaji wa huduma za afya ya uzazi na mtoto ambao ndio lengo kuu la mradi huu.

"KOFIH pia imesaidia kukarabati vituo sita vinavyotoa huduma za upasuaji katika halmashauri hizi pia utolewaji wa huduma za elimu ya afya ya uzazi kwa jamii na mashuleni imeimarika kwa kiasi kikubwa," alisema Moshi.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Kitengo cha Afya na Lishe, Dk. Mageda Luhulya, alieleza faida za mradi ni pamoja na kuhusisha mpango wa damu salama, ujenzi na ukarabati wa vituo vya huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba.

Alisema kuwa Tanzania imekuwa na mabadiliko makubwa katika sekta ya afya kwa sasa na kupelekea vifo vya mama mjamzito na mtoto kupungua kwa kasi, huku akisisitiza ushirikiano wao baina na serikali unakwenda kumaliza tatizo hili kabisa.

# Mufti aunda timu kuchunguza kukithiri kwa ndoa kuvunjika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUFTI Mkuu wa Tanzania, Shehe Abubakar Zubeir ameunda sekretarieti ambayo ameipa jukumu la kufanya utafiti kuhusu sababu za kukithiri kwa uvunjikaji wa ndoa.

Naibu Kadhi Mkuu wa Tanzania, Shehe Ally Ngeruka aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwa niaba ya Mufiti kwenye uzinduzi wa kikundi cha mabalozi wa afya ya akili Tanzania uliofanyika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe jijini hapa.

Alisema ndoa nyingi hivi sasa zinavunjika kwa kiwango ambacho hakitarajiwi wala kutegemewa.

Alisema: "Jambo hilo limemstua sana akaona isije kuwa taarifa anazoletewa ndani yake hazina afya, hebu niunde sekretarieti ambayo itafanya kazi Tanzania nzima kufanya utafiti juu ya suala hili."

Alisema Mufti atakaa na wataalamu baada ya ripoti hiyo ikiwamo wa afya ya akili, wanasaikolojia, wanasheria, wanasiasa na makundi mengine ya kielimu.

"Wataalamu hawa watamshauri Mufti nini kifanyike baada ya hali hii ambayo iko katika jamii,"alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Hospitali ya Mirembe, Dk.Paul Lawala, alisema wamejipanga kuhakikisha elimu ya afya ya jamii inawafikia Watanzania.

"Miongoni mwa wadau wa kijamii ambao tunapanga kushirikiana nao ni watu wanaoshughulika na imani za dini, huko tunapokwenda tutahitaji kuzungumza afya ya akili kwenye kila eneo la jamii,"alisema.

Mwaka 2021 Mkoa wa Dar es Salaam ulisajili migogoro ya ndoa 13,289 kupitia Halmashauri zake ambapo kati yake ndoa 284 zilipeleka migogoro mahakamani.

Aidha, Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Septemba 2022 ilitoa taarifa kuhusu kasi ya kuvunjika kwa ndoa nchini ambapo Mkoa wa Dar es Salaam pekee zaidi ya ndoa 300 zinavunjika kila mwezi.

Matatizo ya kifedha, ukatili ni miongoni mwa mambo yanayotajwa kuchangia kuvunjika kwa ndoa.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi, akikagua banda la mfano wa darasa la elimu ya awali kabla ya kufungua kikao kazi cha makatibu tawala wasaidizi elimu na maofisa elimu wa halmashauri kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# TFRA yaagizwa kudhibiti utoroshaji mbolea ya ruzuku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde ameagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kudhibiti utoroshaji wa mbolea ya ruzuku nje ya nchi ili iwanufaishe watanzania.

Silinde alibainisha hayo jana alipotembelea na kuzungumza na uongozi wa mamlaka hiyo katika ziara iliyolenga kujifunza namna inavyofanya kazi na kutoa maelekezo ya serikali katika kuimarisha utendaji kwa maslahi mapana ya taifa.

Alisema mamlaka hiyo inapaswa kuongeza kasi ya udhibiti wa mbolea hususani katika maeneo ya mipakani ili mbolea ya ruzuku isitoroshwe nje ya nchi.

Aidha, Silinde aliitaka TFRA kuanza zoezi la usambazaji wa mbolea mapema ili kupunguza malalamiko ya kuwafikishia wakulima kwa kuchelewa kama ilivyojitokeza msimu uliopita wa kilimo.

Alisema, mbolea zikipelekwa mapema itawawezesha wakulima kujiandaa mapema kwa kununua na kuhifadhi mbolea majumbani mwao wakisubiri msimu wa kupanda.

"Mbolea iliyopo sasa ianze kusambazwa isisubiri wakati wa msimu ndipo tuanze kukimbizana kupeleka mbolea kwa wakulima," alisema. Katika kuhakikisha ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali inawafikia walengwa, Naibu Waziri Silinde aliitaka TFRA kufanya uhakiki wa taarifa za usajili wa wakulima ili kuondoa tatizo la mawakala kuuza mbolea kwa wakulima waliotoa taarifa za uongo wakati wa usajili.

Hata hivyo aliipongeza mamlaka kwa kuja na mfumo wa ramani unaoiwezesha kuona maeneo walipo mawakala, kiasi cha mbolea walichonacho mawakala wa mbolea kwa nchi nzima na kueleza hiyo itasaidia kufuatilia upatikanaji wa mbolea kwa wakati katika maeneo yote.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku, Louis Kasera alisema utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima kumeamsha ari ya wakulima wengi kutumia mbolea katika kilimo chao na hivyo uhitaji wa bidhaa hiyo kuwa mkubwa.

Alisema mamlaka imetatua kero ya usambazaji iliyojitokeza msimu uliopita wa kilimo kwa kusajili vyama vya ushirika 198 nchi nzima na vyama vidogo vya ushirika zaidi ya 2,000 vitakavyosaidia kufikisha mbolea kwa wakulima wao hata katika maeneo ya pembezoni.

Kasera alisema lengo la mamlaka ni kumwezesha mkulima asitembee zaidi ya umbali wa kilomita 15 kwenda kutafuta mbolea na hivyo wamepanga bei elekezi kulingana na eneo ambalo mbolea inafika.

Louis alisema mamlaka imeboresha mfumo ambapo kila mfuko wa mbolea utakaouzwa namba ya siri itakayokuwa imetumika haitatumika tena na mkulima atapokea namba nyingine itakayomruhusu kununua mbolea kulingana na ukubwa wa shamba alioandikisha wakati wa usajili.





# NEMC kusimamia ujenzi wa Barabara Katumba-Lupaso

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema litasimamia ujenzi wa Barabara ya Katumba-Lupaso (km 35) wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya yenye urefu wa Km. 35 ili kuhakikisha hauathiri mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samwel Gwamaka aliyasema hayo juzi alipoambatana na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Innocent Bashungwa pamoja na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba kwenye ukaguzi wa barabara hiyo ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami.

Barabara hiyo ni sehemu ya Barabara ya Katumba -Lwangwa - Mbambo -Tukuyu yenye urefu wa zaidi ya Km. 80 ambayo inaunganisha Halmashauri za Rungwe na Busokelo.

Alisema barabara hiyo inapita kwenye baadhi ya maeneo ya vyanzo vya maji na mito inayotiririsha maji yake kuelekea Ziwa Nyasa na hivyo ni lazima wahakikishe ujenzi wake hauathiri vyanzo hivyo ambavyo ni muhimu kwa ustawi wa binadamu na viumbe wengine.

Alisema watashirikiana na uongozi wa Bonde la Ziwa Nyasa ambao ndio wasimamizi wa vyanzo vya maji vilivyopo kwenye eneo pamoja na rasilimali za maji.

"Miradi hii ya barabara huwa inafanyiwa Tathimini ya Athari za Kimazingira (EIA) na tunakuwa makini zaidi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji, tusipovilinda vyanzo hivi vitakauka na hata kina cha ziwa letu kitapungua na hivyo kutusababishia tatizo la uhaba wa maji," alisema Dk. Gwamaka na kuongeza.

"Sisi kama wasimamizi wa mazingira tutahakikisha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inafuatwa kwenye utekelezaji wa mradi huu pamoja na miradi mingine yote," aliongeza.

Vilevile, alisema maeneo mengi ambayo barabara hiyo inapita ni jirani na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambayo pia inatakiwa kulindwa ili isiharibiwe na shughuli za kibinadamu.

Aidha, aliipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kuamua kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa maelezo kuwa ni muhimu kwa ajili ya wananchi kusafirisha mazao mbalimbali ambayo wanazalisha kwenye eneo hilo.

Akizungumza na wananchi wa Bonde la Mwakaleli, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Bashungwa alisema barabara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025.

Alisema fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo zipo na mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi kwa kuanza na kipande hicho cha Katumba-Lupaso ambacho kitasaidia pia kuwanganisha wananchi wa Busokelo na Wilaya ya Makete mkoani Njombe.

"Lengo la serikali ni kuunganisha nchi nzima kwa barabara za lami, hii barabara ni sehemu ya barabara muhimu ambazo serikali iliwaahidi wananchi, tutasimamia ili kuhakikisha inajengwa kwa viwango vinavyostahili," alisema Bashungwa.

Waziri wa Fedha, Dk. Nchemba alisema atahakikisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo zinatoka kwa wakati ili barabara hiyo ikamilike kwa wakati.

Aliwaomba wananchi wa maeneo yote ambayo barabara hiyo inapita kuhakikisha wanailinda miundombinu ya barabara hiyo ili iwasaidie kwa muda mrefu zaidi.

## Wanafunzi waiangukia CCM kujengewa bwalo la chakula

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Yakobi iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, wameiomba serikali kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwajengea bwalo ambalo watalitumia kwa ajili ya chakula, mikutano pamoja na kufanyia mitihani.

Ombi hilo walilitoa mbele ya Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Njombe ambapo walisema kukosekana kwa bwalo kunasababisha kulia chakula nje ama kwenye vyumba vya madarasa.

"Hapa shuleni kuna changamoto ya bwalo la kulia chakula, wametujengea jiko tu kwahiyo tunakaa nje humu humu na madarasani" alisema Victoria Mkini.

Zakaria Kaduma alisema muda wa ugawaji chakula wanafunzi wanalazimika wachukue chakula jikoni ili wakalie madarasani au mabwenini kwa sababu bwalo la kulia chakula hakuna.

"Tunaiomba serikali itufikirie, itujengee bwalo ili tuweze kula chakula sehemu nzuri" alisema Kaduma.

Akijibu changamoto hiyo Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Thadei Luoga, alisema wameichukua changamoto hiyo na Oktoba 15 fedha zitaanza kuletwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Akizungumza na wanafunzi hao Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe, Julias Peter, aliwataka wanafunzi kuongeza bidii katika masomo yao, sambamba na kutunza miundombinu shuleni hapo.

Peter alisema fedha ambazo zinaletwa kwa ajili ya kujenga majengo mazuri lengo ni kuinua kiwago cha elimu nchini.

Katibu huyo alisema serikali itaendelea kutatua changamoto zote ambazo ni kero ili wananchi waendelee kuiamini CCM.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Njombe, Samwel Mgaya alisema nia ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona kwamba katika uchaguzi wa serikali za mitaa hadi uchaguzi mkuu wanachagua viongozi wanaotokana wa CCM ili kumpa urahisi katika kutekeleza masuala ya kimaendeleo.



Baadhi ya vijana wa Mkoa wa Mbeya wakifuatilia mafunzo ya ujasiriamali yaliyoandaliwa na seneti ya vyuo na vyuo vikuu vya mkoa huo katika Chuo cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mradi wa maji wakwama miaka mitatu, wananchi 'wafura'

**Na Nebart Msokwa,**
SONGWE

WANANCHI wa Kata ya Kanga wilayani Songwe wamekerwa baada ya Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa kutokamilisha mradi wa maji wa kata hiyo kwa zaidi ya miaka mitatu licha ya serikali kutoa fedha.

Aidha, wananchi hao wamesema afya zao ziko hatarini kutokana na kutumia maji ambayo usalama wake ni wa mashaka hasa kipindi cha kiangazi ambacho wanalazimika kutumia maji ya kwenye vijito.

Walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe, Neema Mwandabila na kamati ya utekelezaji ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Songwe.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kanga, Mwalimu Leonard Mpoli alisema shule hiyo ni moja ya maeneo ambayo yanaathirika na tatizo la maji kwa kutokuwa na huduma hiyo kabisa hali ambayo inawalazimu wanafunzi kwenda kuchota mtoni.

Alisema shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi 800 lakini haina huduma ya maji hali ambayo inahatarisha afya za wanafunzi pamoja na watumishi wa shule.

"Hapa hatuna kisima wala maji ya bomba lakini kama unavyoona tuna wanafunzi wengi, tatizo kubwa zaidi hapa ni kwa mabinti zetu ambao muda wote wanatakiwa kuwa wasafi kutokana na mazingira yao," alisema Mwalimu Mpoli.

Diwani wa Kata hiyo, Erick Kihinda alisema kero ya maji katika kata yake ni kubwa na hajui sababu za mradi wa maji ambao serikali ilitoa fedha haukamiliki kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Alisema fedha zote za mradi zililipwa kwa mkandarasi lakini mpaka leo hawajakabidhiwa mradi huo na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kufuatilia.

Akijibu kero hiyo Mbunge wa Viti Maalumu, Neema Mwandabila alisema atafuatilia zaidi ili kujua sababu za mradi huo kutokamilika licha ya serikali kutoa fedha lakini Wilaya ya Songwe maeneo mengi hayana huduma hiyo.

Alisema yeye pamoja na wabunge wenzake wa Mkoa wa Songwe wamekuwa wakipigania kuhakikisha wananchi wanapata huduma lakini wanakwamishwa na watu wachache.

"Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Naibu wake Mhandisi Maryprisca Mahundi wanapambana kuhakikisha wananchi wanapata maji maeneo mbalimbali nchini, hivyo nitawaomba watuangalie na sisi huku Songwe kwa jicho la kipekee," alisema Neema.

Aliahidi pia kutembelea Ofisi ya RUWASA Wilaya ya Songwe ili kufahamu sababu ya mradi huo kutokamilika kwa wakati ilihali serikali ilishatoa fedha za ujenzi.





## Benki ya Uwekezaji kuanzishwa kuwasaidia w'biashara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema ipo katika mchakato wa kuanzisha Benki ya Uwekezaji ili kusaidia wafanyabiashara katika sekta binafsi wawekeze katika miradi ya kiuchumi na maendeleo.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi (CCM), Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua lini serikali itaanzisha Benki ya Uwekezaji kwa ajili ya kusaidia mitaji katika sekta binafsi.

Ameir alisema malengo makubwa ya kuwepo kwa Benki ya Uwekezaji nchini ni kufungua milango kwa wawekezaji ikiwemo wazalendo kupata mikopo kutoka taasisi za kibenki kwa ajili ya kuendesha shughuli zao ikiwemo miradi.

Alisema hatua za kuanzishwa kwa benki hiyo zimeanza kuchukuliwa ikiwamo kuandaa andiko la dhana ambapo hatua inayofuata ni kutayarisha uchambuzi yakinifu wa dhana hiyo.

Aidha, alizitaja hatua nyingine ikiwamo mazungumzo yameanza kufanyika kwa taasisi za kifedha na watu binafsi kwa namna ambapo wanaweza kuwahusisha wafanyabiashara binafsi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafuatilia kwa karibu suala hilo kwa lengo la kuwa na taasisi ya fedha ambayo itasaidia na kutoa mikopo kwa sekta binafsi katika kuendesha biashara zao.

Alisema ifikapo mwaka 2025 uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji utakuwa tayari umekamilika na kuanza kufanya kazi zake ikiwamo kutoa mikopo kwa sekta binafsi.

Alisema: "Hiyo ndiyo mikakati yetu kuona kwamba ifikapo mwaka 2025 tunaanzisha Benki ya Uwekezaji Zanzibar ambayo tunaamini kwa kiasi kikubwa itakuwa mkombozi katika kukuza na kusaidia sekta binafsi kupiga hatua kubwa ya maendeleo".

**Alisema ifikapo mwaka 2025 uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji utakuwa tayari umekamilika na kuanza kufanya kazi zake ikiwamo kutoa mikopo kwa sekta binafsi.**

# Serikali yajinasibu kuondoa urasimu sekta ya uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imefanikiwa kufanya maboresho makubwa katika Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA) ikiwamo kuondosha urasimu katika sekta ya uwekezaji, hatua ambayo imeifanya mamlaka kukamilisha taratibu zote za kutoa cheti kwa wawekezaji katika kipindi kifupi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya mashirika na taasisi mbalimbali kutoka China ikiwa ni juhudi za kuwavutia wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuwekeza Zanzibar.

Soraga alisema serikali imechukua hatua za makusudi ikiwamo kufungua milango katika sekta ya uwekezaji na kufanya marekebisho makubwa ya sheria zake ikiwamo za Mamlaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji Zanzibar ambayo sasa ni kituo kimoja cha uwekezaji nchini.

''Tunawakaribisha wawekezaji waje nchini kuwekeza....mazingira ya uwekezaji Zanzibar yameimarishwa na kuondosha urasimu uliokuwapo awali ambapo Mamlaka ya Uwekezaji ZIPA sasa ni kituo kimoja cha uwekezaji ambapo mwekezaji anaweza kukamilisha mambo yote katika kipindi cha siku tatu tu," alisema Soraga.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar, Sharif Ali Sharif, alisema kampuni tofauti ya uwekezaji ikiwamo ya mawasiliano imeonesha nia ya kuwekeza Zanzibar kufuatia mazingira mazuri yaliopo ambayo yameondoa urasimu.

"Tumefanikiwa kuboresha mazingira ya uwekezaji Zanzibar na ndiyo maana tunashuhudia utiaji wa saini wa makubaliano ya kuimarisha biashara kati ya China na Zanzibar," alisema Sharif.

Baadhi ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wawekezaji kutoka China ni kukuza sekta ya biashara kati ya Jimbo la Weihai Wendeng pamoja na Taasisi ya Biashara ya China kwa ajili ya kurahisisha biashara katika Jimbo la Shanghai China na Zanzibar.



Baadhi ya wazee wakifuatilia hotuba katika Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Chanzo kuchelewa kwa hukumu kesi dawa za kulevya chatajwa

**Na Rahma Suleimman,**
ZANZIBAR

KUCHELEWA kutolewa hukumu kwa kesi za dawa za kulevya kunatokana na kukosekana kwa ushahidi usiokuwa na shaka, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa mrundikano mkubwa wa kesi hizo mahakamani.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Viti Maalumu wanawake, Mwanaidi Kassim Mussa aliyetaka kujua sababu za kuchelewa kwa kesi za dawa za kulevya katika Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Suleiman alizitaja sababu tatu zinazosababisha kuchelewa kusikilizwa kesi hizo mahakamani ikiwamo kukosekana kwa ushahidi uliokamilika usiokuwa na shaka ambao utawatia hatiani watuhumiwa.

Alisema wakati mwingine ushahidi unaotolewa kwa watuhumiwa haujakamilika vizuri kiasi cha kuwatia hatiani wahusika na wakati mwingine upande wa mashahidi hawapo tayari kutoa ushahidi pamoja na kufika mahakamani.

Aidha, alizitaja sababu nyingine zinazosababisha kuchelewa kusikilizwa kwa kesi hizo na kutolewa uamuzi wake ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Dawa za Kulevya ambapo kwa sasa kesi hizo husikilizwa katika Mahakama Kuu tu.

Alizitaja sababu nyingine zinazosababisha kuchelewa kusikilizwa kwa kesi mahakamani ni kukosekana kwa wataalamu wa kutosha kutoa ushahidi ikiwamo wafanyakazi wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Hizo ndiyo sababu kuu zinazosababisha kuchelewa kusikilizwa kesi za dawa za kulevya katika mahakama zetu na matokeo yake huchukua muda mrefu kusikilizwa," alisema.

Hata hivyo Suleiman aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba juhudi kubwa zinafanyika katika kupunguza msongamano wa kesi Mahakama Kuu ambapo kwa sasa kesi zinasikilizwa kwa wastani miezi nane kutoka miaka miwili.

Alisema: "Mheshimiwa Spika tumepiga hatua katika kupunguza msongamano wa kesi mahakamani ambapo kwa sasa wastani wa kesi miezi 8 zinasikilizwa baada ya miaka miwili."

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



EMANUEL ROBIAM NDOSA anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S5391/0045/2019 kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL mwaka 2019.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/4181/2023

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

CHARLES PETER MOLLEL anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T 768 BKN, CHASSIS NAMBA: JI00G005960 na ENGINE NAMBA: HC0607808. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/MOLLEL

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

NDUGU SARAH MAGENI SANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI T354 CWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE. POLISI TAARIFA MKT/RB/584/2021.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ABEL MARCO PALLANGYO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI, GARI LENYE NAMBA ZA USAJILI T 411 AVE AINA YA TOYOTA Gaia ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI MWA/MAG/RB/190800/2023


## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



SALUMU SELEMANI MKONDA anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 063258 iliyotolewa makao makuu Dar es Salaam PCO mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/TEM/20211/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**USIMAMIZI WA MIRATHI Na......23/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU BAKARI MOHAMED MLAPAKOLO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA MWASITI BAKARI MOHAMED**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(20ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika Shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi 10 Mwaka 2023,kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.
ZINGATIA:
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
Marehemu hakuacha Wosia
Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 9 mwaka 2023



## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

SIMON GODLISTEN LAIZER anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la umiliki WATER SOLUTION DILLING CO. LTD yenye namba za usajili T 686 AGC aina ya TOYOTA RAV 4. Chassis No. SXA10054071. Engine No. 3S1824416. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: PHQ/ARU/ARU/3050/2023.

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wagunduzi chanjo Uviko-19 watwaa Tuzo ya Nobel

**Oslo,** NORWAY

TUZO ya Nobel ya Dawa ya mwaka 2023 imetuzwa kwa wanasayansi wawili, kutokana na uvumbuzi wa chanjo za Uviko-19 aina ya mRNA.

Kamati inayotoa tuzo hizo imesema, Kataline Kariko na Drew Weissman, walipiga hatua muhimu wakati wa janga la corona.

Kariko ni profesa kwenye Chuo Kikuu cha Szeged pia kwenye Chuo cha Afya cha Perelman huko Chuo Kikuu cha Pennsylvania.

**Tuzo ya Nobel ya Dawa, siku zote huwa ya kwanza kutolewa miongoni mwa nyingine kila mwaka.**

Weissmana, ni profesa kwenye Chuo cha Utafiti wa Chanjo cha Roberts Family na pia Mkurugenzi wa Chuo cha RNA Innovations huko Pennsylvania.

Tuzo ya Nobel ya Dawa, siku zote huwa ya kwanza kutolewa miongoni mwa nyingine kila mwaka.

Tuzo za Fizikia, Kemia, Fasihi, Amani na Uchumi zitatangazwa kila siku, hadi Oktoba 9, mwaka huu.

Alfred Nobel, mwanzilishi wa tuzo hizo alikuwa mfanyabiashara katika karne ya 19 na ambaye alijipatia utajiri mkubwa, baada ya kugundua dynamite.

Tuzo ya kwanza ya Nobel, ilitolewa 1901 miaka mitano baada ya kifo chake. **VOA**





Wanasayansi Kataline Kariko na Drew Weissman. **PICHA: MTANDAO**

## Paa la kanisa laua makumi

**Mexico City,** MEXICO

WATU 10 wameripotiwa kuuawa na wengine 20 wamenaswa, baada ya paa la kanisa kuporomoka.

Vyombo vya habari vilisema watu 49 walipelekwa hospitalini, baada ya paa la kanisa la Ciudad Madero la Santa Cruz kuanguka.

Polisi katika jimbo la pwani la Tamaulipas, walisema karibu watu 100 walikuwa kwenye misa wakati wa tukio hilo. Vyombo vya habari vya ndani viliripoti kuwa misa hiyo ilikuwa hafla ya ubatizo.

Watoto kadhaa wanaaminika kuwa miongoni mwa walionaswa na juhudi za kuwaokoa zinaendelea.

Picha kwenye mitandao ya kijamii zilionesha jengo la kanisa likiwa magofu, huku watu wakizingira vifusi, wakitafuta waliokuwa wamenaswa ndani.

Askofu wa Dayosisi ya Tampico, José Armando Álvarez Cano, alituma ujumbe kwa jamii kwenye mitandao ya kijamii akisema, kazi inaendelea "kuwatafuta walio chini ya vifusi. **BBC**

## Watu 40 wajeruhiwa kwa moto

**Ismailia,** MISRI

TAKRIBAN watu 40 wamejeruhiwa katika kisa cha moto, ulioteketeza moja ya majengo makubwa katika mji wa Ismailia nchini Misri, ukingo wa magharibi wa mfereji wa Suez.

Moto huo umetokea jana, ambao chanzo chake bado hakikujulikana. Ulizuka katika makao makuu ya Kurugenzi ya Usalama.

Kwenye mitandao ya kijamii, picha nyingi zilizorushwa mtandaoni zinaonesha miale mikali ikiteketeza ghorofa nyingi za jengo hilo kubwa la mawe, ambamo huishi askari.

Kati ya majeruhi 26 waliopelekwa hospitali ya eneo hilo, kwa mujibu wa Wizara ya Afya, 24 wanasumbuliwa na kukosa hewa na wawili wameungua sana. Wengine 12 walitibiwa katika eneo la tukio.

Wizara ya Afya imetuma magari ya wagonjwa 50 kwenye eneo la tukio, pamoja na maofisa wa Idara ya Huduma za Dharura za Kijeshi, ikiwa ni pamoja na ndege mbili. **RFI**



## Tshisekedi, Fayulu kukutana tena Desemba

**Kinshasa,** DRC

RAIS Felix Tshisekedi anagombania muhula wa pili katika taifa lenye utajiri mkuu wa cobalt duniani, baada ya kushinda wa kwanza uliokuwa na utata mwaka 2018.

Wajumbe wa Muungano wa Union Sacree, unaohusisha wanasiasa maarufu wa Congo kama Waziri wa Ulinzi, Jean Pierre Bemba na Waziri wa Uchumi, Vital Kamerhe, walimchagua Tshisekedi kwa sauti moja.

Utawala wake umekumbwa na hali ngumu ya uchumi, janga la Uviko-19, mlipuko wa ebola, ukosefu wa usalama hasa mashariki ya nchi, ambako wapiganaji wa kundi la M23 waliteka sehemu ya maeneo na kusababisha kuvunjika kwa uhusiano na Rwanda.

Tshisekedi, kijana wa mwanasiasa mashuhuri wa upinzani Etienne Tshisekedi, aliyeahidi kupambana na ulaji rushwa na utawala wa kimabavu anakanusha tuhuma kutoka makundi ya kutetea haki za binadamu na wakosoaji wake, kwamba ameshindwa kutekeleza ahadi zake.

Kiongozi wa upinzani Martin Fayulu aliyeshindwa dhidi ya Tshisekedi mwaka 2018, alithibitisha kwamba, atawania tena kiti cha urais, baada ya awali kutishia kususia uchaguzi, ili kulalamikia ubaridhirifu unaotokea katika kuandikishwa kwa wapigakura. **VOA**

## Kenya yafunga vituo kulelea yatima

**Nairobi,** KENYA

SERIKALI imetangaza kufunga nyumba zote za watoto zinazomilikiwa na watu binafsi ndani ya miaka minane, ikisema hilo litasaidia kwa kiasi kukomesha ulanguzi wa watoto.

"Katika miaka minane ijayo nyumba za kibinafsi hazitakuwapo."

"Tunahitaji kujiandaa, ili kuwaweka mazingira mazuri kwa watoto ambao watatoka katika nyumba za kibinafsi," Waziri wa Kazi na Ulinzi wa Jamii, Florence Bore, alisema hayo katika hafla juzi.

Bore alikuwa amechapisha kwenye ujumbe huo kwenye mtandao wa X kwamba serikali tayari ilikuwa katika harakati za kufunga nyumba za watoto na yatima.

Alisema watoto katika taasisi hizo, watawekwa katika malezi ya familia na jamii, jambo ambalo litatoa mazingira bora kwa watoto hao.

Wenyeji wanasema kuna zaidi ya watoto 40,000 katika nyumba 800 za kulea nchini Kenya.

Kenya, imekuwa ikitafuta mbinu ya kuondoa nyumba za binafsi za watoto na watoto yatima, tangu kupitishwa kwa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2022, ambayo inataka mabadiliko ya ulezi, uwekaji wa malezi na kuasili. **BBC**

# SINGIDA FG YAJILAUMU YENYEWE IKITOA SABABU KIPIGO SHIRIKISHO

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa jumla ya mabao 4-2 na Future FC, benchi la ufundi la Klabu ya Singida Fountain Gate limeomba radhi kwa Watanzania kwa kushindwa kufuzu hatua ya makundi.

**Singida FG, ilishindwa kutumia fursa ya wapinzani wao kucheza pungufu kwa dakika 35 baada ya beki wa kati wa Future FC, Mahmoud Rizk, kuonyeshwa kadi nyekundu dakika ya 55.**

Wakati Rizk akitolewa wenyeji walikuwa mbele kwa mabao 2-1, lakini bado Singida FG ilielemewa na kujikuta ikitandikwa mengine mawili na mchezo kumalizika kwa Future kuibuka na ushindi wa mabao 4-1, hivyo kutinga hatua ya makundi kwa mabao 4-2 kutokana na mchezo wa awali hapa nchini kupoteza kwa bao 1-0.

Akizungumza kwa masikitiko baada ya kumalizika kwa mchezo huo jijini Cairo, Misri Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ramadhan Nsanzurwimo, alisema matokeo hayo yamemuumiza kwa kiasi kikubwa kwani walikuwa na kila sababu ya kufuzu.

"Ninaomba radhi kwa Watanzania kwa hiki kilichotokea, tulikuwa tunastahili kufuzu, isipokuwa tumefanya makosa ambayo wapinzani wetu wameyatumia wakafanikiwa kusonga mbele, inauma kwani sikutegemea matokeo haya," alisema Nsanzurwimo.

Kuhusu mchezo huo wa marudiano, Nsanzurwimo alisema ulikuwa mzuri na kwamba kipindi cha kwanza timu yake ilicheza vizuri tofauti na kipindi cha pili ambacho wenyeji walikuwa pungufu, lakini kikosi chake kilijikuta kikipoteza umakini na kuwapa nafasi wapinzani wao kuwaadhibu.

"Kipindi cha kwanza timu yangu ilicheza vizuri, hakukuwa na makosa mengi kama cha pili, timu ilipoteza umakini kwa makosa ya mchezaji mmoja mmoja ambayo mpinzani wetu alitumia nafasi hiyo kutufunga," alisema.

Alisema, sababu nyingine iliyowafanya washindwe kupata matokeo kipindi hicho cha pili ni wachezaji wake kukaba kwa macho kitu ambacho si rahisi kumthibiti mpinzani kwa kwa njia hiyo.

"Wenzetu walikaba na kutumia mshambuliaji mmoja, lakini sisi tulikaba kwa kutumia walinzi wanne kwa ufupi walikaba kwa macho," alisema.

Alisema kwa sasa wanarudi nyumbani kwa ajili ya kujipanga kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar unaotarajiwa kuchezwa keshokutwa, Jumatano.

Wakati huo huo, rais wa Klabu hiyo, Japhet Makau, amesema wanarudi kujipanga kuhakikisha wanaboresha benchi la ufundi pamoja na kusajili wachezaji wenye uzoefu zaidi.

"Tunasikitika hatukuweza kutimiza malengo yetu ya kuingia hatua ya makundi kwenye mechi za kimataifa, timu inatakiwa ifanye maandalizi ya muda mrefu vile vile tunatakiwa tuwe na benchi la ufundi ambalo lina uzoefu na michuano kama hii pamoja na wachezaji wazuri ili ifikapo msimu ujao tufanye vizuri zaidi," alisema Makau.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akikabidhiwa jezi ya Al Ahly na kiongozi wa klabu hiyo wiki iliyopita baada ya kufanya ziara klabuni hapo kuona uwekezaji iliyoufanya jijini Cairo, Misri. Ndumbaro pia aliikaribisha Al Ahly kuja kuwekeza katika sekta ya michezo hapa nchini kwa kufungua Academy ya michezo. **PICHA: WUSM**

# Mtoko Kibingwa msimu wa sita wazinduliwa

**Mwandishi Wetu**

MSIMU wa sita wa Promosheni ya Betika 'Mtoko wa Kibingwa' umezinduliwa jana, ukitoa fursa kwa mashabiki 50 wa soka nchini kuishuhudia dabi ya Simba na Yanga kwa gharama za Betika.

Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Rugambwa Juvenalius, amesema washindi wa droo za promosheni hiyo iliyozinduliwa jana watatangazwa Oktoba 11, 18 na 25 na wale wa mwisho itakuwa ni Novemba Mosi, mwaka huu tayari kuishuhudia dabi hiyo.

"Washindi 50 watapata fursa ya kuishuhudia dabi ya Simba na Yanga ya Ligi Kuu Novemba," alisema Rugambwa aliyekuwa sambamba na meneja mkuu wa Betika, Tanzania jana.

Alisema, "ili kushinda, unaweka mkeka kwenye mechi kuanzia tatu kwa dau la Sh. 2,000 au zaidi.

"Kila wiki washindi zaidi ya 10 watatangazwa, pia fursa hii itawahusisha wachezaji wa Kitonga Jackpot," alisema Rugambwa huku akizipongeza Simba na Yanga kutinga hatua ya makundi kwenye mashindano ya Kimataifa ya Caf.

"Hii inazidi kukoleza utamu wa dabi, itakuwa mechi nzuri na isiyotabirika kwa timu zote," alisema na kuongeza.

"Huu ni msimu wa sita kwa promosheni hiyo ya Mtoko wa Kibingwa ambayo inatoa fursa kwa mashabiki wa Simba na Yanga kuishuhudia dabi hiyo laivu kwa hadhi ya nyota tano.

"Kwa wale wa mikoani, watasafiri kwa ndege, washindi wote watalala kwenye hoteli ya nyota tano, watakwenda uwanjani kwa king'ora na kuishuhudia dabi wakiwa jukwaa la VIP, gharama zote zikiwa chini ya Betika," alisema.

Alisema msimu huu kaulimbiu ya Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa ni Shinda bila Miyeyusho.

"Msimu uliopita, tulikuwa na matukio tofauti ikiwamo pati la 'bata ya msimu', wakati huu tutakuwa na mambo mazuri zaidi kwa mabingwa watakaobashiri kwenye Mtoko wa Kibingwa kupitia Betika," alisema.

## Kaze apania ushindi kwa Kagera Sugar

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA mchezo wa kesho wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa Klabu ya Namungo, Cedric Kaze, amesema ameimarisha safu yake ya ushambuliaji kuhakikisha hawapotezi.

Akizungumza na gazeti hili jana wakiwa njiani kuelekea Bukoba, alisema hana wasiwasi kwani makosa aliyoyaona kwenye mchezo uliopita ameyafanyia kazi.

"Kwa sasa timu yangu ipo vizuri nimefanya maandalizi ya kutosha ili tuweze kupata matokeo katika mchezo huo," alisema Kaze.

Alisema wachezaji wote wanaendelea vema kiafya isipokuwa Paterne Counou ambao atakosekana kutokana na kuwa majeruhi.

Aliongeza kuwa anaiheshimu timu ya Kagera Sugar kwani ina wachezaji wenye uzoefu, hivyo wanapaswa kuingia kwa tahadhari kubwa ili kupata matokeo mazuri.

## New City yaanika kinachoiliza Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa timu ya New City, Razak Salum amesema ugeni wao kwenye Ligi Kuu Zanzibar ndio unaowasumbua na kusababisha kufanya vibaya katika michezo minne waliyocheza.

New City FC inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama moja katika michezo minne iliyocheza.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema bado kikosi chake kinasumbuliwa na ugeni wa Ligi Kuu, jambo ambalo sasa anataka kulibadili kwa mbinu mbadala ili kupata matokeo.

Alisema timu yake inawachezaji wazuri na inacheza mpira mzuri ila wanashindwa kuzitumia nafasi wanazotengeneza ili kupata magoli.

Alisema katika michezo yote waliyocheza mapungufu makubwa aliyoyaona ni wachezaji kushindwa kutumia nafasi hasa wanapokuwa wanashambulia katika lango la wapinzani.

"Kama unafuatilia michezo yetu, timu inacheza vizuri, wachezaji wanakaa na mpira kwa muda mrefu, lakini katika suala la kufunga hapo ndipo tatizo, nikiri kuwa wachezaji wangu wanapoteza umakini hivyo hii ni ya kufanyia kazi," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN, TONEY NA CHELSEA

MATUMIZI makubwa ya Chelsea yanatazamiwa kuendelea Januari huku klabu hiyo ikimlenga mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 24, Victor Osimhen na mshambuliaji wa Brentford wa England, Ivan Toney, 27. ***(Guardian)***

### MILIONI 500 ZATAFUTWA

KLABU ya Chelsea pia inatafuta mkopo wa pauni milioni 500 ili kufadhili usajili huo baada ya kutumia pauni bilioni moja katika kipindi cha madirisha matatu ya uhamisho. ***(Sun)***

### YAMGEUKIA PHILLIPS

KLABU ya Arsenal itamgeukia kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, 27, katika dirisha la Januari huku 'Washikabunduki' hao wakipania kuimarisha safu yao ya kati. ***(Fichajes)***

### YAMAL MKATABA MPYA

WINGA wa Barcelona mwenye umri wa miaka 16 raia wa Hispania, Lamine Yamal, anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na klabu hiyo, ambao una kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni bilioni moja. ***(Fabrizio Romano)***

### NEWCASTLE KWA ANDERSON

KLABU ya Newcastle inamfuatilia mlinzi wa Crystal Palace raia wa Denmark, Joachim Andersen, 27, kwa nia ya kumnunua mchezaji huyo 27 Januari. ***(Football Insider)***

### BARCA KUMUUZA FATI

BARCELONA iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati, 20, msimu ujao wa majira ya joto baada ya mchezaji huyo kumaliza muda wake wa mkopo Brighton. ***(Sport)***

### MESSI AMTAKA MODRIC

LIONEL Messi ameitaka Inter Miami kumsajili kiungo wa kati wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric, 38. ***(Cadena Ser)***

### ALEXANDER-ARNOLD JUU

LIVERPOOL imekubaliana kimsingi na beki wa England, Trent Alexander-Arnold, 24, kwa mkataba mpya, ambao utamfanya mchezaji huyo kulipwa zaidi ya pauni 200,000 kwa wiki, pamoja na bonasi. ***(Football Insider)***

### MOSCARDO AWINDWA BARCA

BARCELONA imeanza mazungumzo na Corinthians kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Brazil, Gabriel Moscardo, 18, huku wakitarajia kuipiku Chelsea kwenye usajili wake.***(Sport via Goal)***

### RABIOT MKATABA MPYA

KLABU ya Juventus inatumaini kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28, baada ya kukataa kuhamia Manchester United msimu wa majira ya joto. ***(Tuttosport)***

### TAPSOBA ATAJWA SPURS

KLABU ya Tottenham inataka kumsajili beki wa Bayern Leverkusen mwenye umri wa miaka 24 raia wa Burkina Faso, Edmond Tapsoba. ***(Fichajes)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI [...]



# LISANDRO MARTINEZ APASULIWA TENA

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa Manchester United, Lisandro Martinez, amefanyiwa tena upasuaji wa mguu wake kujaribu kutatua tatizo la mara kwa mara.

**Martinez alipasuka mfupa wa mguu kwa mara ya kwanza wakati wa mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Europa ya 'Mashetani Wekundu' hao dhidi ya Sevilla msimu uliopita.**

Aliendelea kukosa miezi miwili ya mwisho ya msimu. Ingawa aliweza kurejea kwa mechi za kabla ya msimu mpya na mechi za ufunguzi za United za kampeni ya 2023/24, klabu hiyo ilithibitisha Ijumaa kwamba alikuwa na jeraha la kujirudia na angekabiliwa na kipindi kisichojulikana cha kukaa nje ya uwanja.

Gazeti la Daily Mail sasa liliripoti kuwa Martinez jana Jumatatu alitarajiwa kufanyiwa upasuaji ili kutatua tatizo hilo na atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu ijayo, ikimaanisha kuwa hakuna uwezekano wa kucheza tena kwa mwaka huu.

Ripoti hiyo inaongeza kuwa baada ya United kuchapwa mabao 3-1 na Arsenal kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa Septemba, mwaka huu, alitumia dawa za kutuliza maumivu ili kucheza katika kichapo kutoka kwa Brighton & Hove Albion na kisha Bayern Munich.

Baada ya kufanyiwa vipimo zaidi wiki hii, United waligundua mguu wa Martinez haujapona ipasavyo na upasuaji zaidi ungehitajika kurekebisha.

**Ni habari ya kusikitisha na kukatisha tamaa, kikosi kitamkosa...**

Kocha wa Man United, Erik ten Hag alionesha huruma kwa beki wake nyota baada ya kujua angekosa kipindi kingine kirefu.

"Hiyo ni habari ya kusikitisha na ya kukatisha tamaa," alisema Ten Hag akiiambia MUTV.

"Lazima apitie utaratibu huo huo na ninampa pole sana.

"Kikosi kitamkosa, kama unavyojua, tuna majeruhi wengi zaidi, hivyo ni lazima tukabiliane nayo kama kikosi, kama klabu tunatakiwa kukabiliana na majeruhi.

"Lazima awe na nguvu. Atapambana, nina uhakika. Ni mhusika.

"Bado kuna msimu mrefu mbele na atakuwa fiti. Tunapaswa kufanya kazi yetu, kujiweka katika nafasi nzuri, ili aweze kuchangia, na kuongeza ubora, atakaporejea."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 728,

MECHI KALI
DODOMA FC
VERSUS
AZAM FC
1 | 4.15
X | 3.21
2 | 1.86

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MWANASHERIA AFICHUA SALAH ANAZOA PAUNI MILIONI MOJA



**LIVERPOOL,** England

MWANASHERIA na mshauri wa Mohamed Salah amedokeza kuwa nyota huyo wa Liverpool anaweza kuwa anapata kiasi kikubwa mno cha mapato ya jumla kwa mujibu wa The Guardian.

Rammy Abbas Issa aliripotiwa kuwaambia watafiti wa Shule ya Biashara ya Harvard (Harvard Business School (HBS) kwamba kiasi hicho cha fedha kitakuwa matarajio 'ya kihafidhina' kwa nyota huyo wa Misri.

Issa pia alifunguka jinsi Salah alivyokaribia kuondoka kwa wababe hao wa Ligi Kuu kabla ya kuweka mustakabali wake klabuni hapo kwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu.

Salah alikuwa ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na kulikuwa na wasiwasi kwamba angeondoka baada ya miezi kadhaa ya mazungumzo kushindikana. Lakini, fowadi huyo wa Misri alisaini mkataba mpya Julai 2022 - akijitolea kukaa hapo Liverpool hadi Juni 2025.

Issa sasa amefichua kwamba mkataba mpya wa Salah pamoja na stahiki nyingine utamfanya apate pauni milioni moja kwa wiki. Kwa mujibu wa The Guardian, Issa alisema: "Unapokuwa umeweka maombi yako mezani na hupati chochote ulichoomba, unapaswa kuanza kufikiria kuhusu kuachana."

Wakati huo huo, Salah mwenyewe alinukuliwa akisema alianza kuona mambo 'tofauti' baada ya Liverpool kukataa maombi yake yote.

# Juve yapambana kumbakisha Rabio



**TURIN,** Italia

JUVENTUS inafanyia kazi mkataba mpya wa muda mrefu wa kiungo wa kati Mfaransa Adrien Rabiot baada ya kumshawishi kubakia hapo Turin wakati wa majira ya joto.

Manchester United ilijaribu kumsajili wakati wa dirisha la usajili, lakini walikataliwa na kiungo huyo ambaye aliamua kuongeza muda wake Juventus.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alikubali mkataba wa mwaka mmoja na miamba hao wa Serie A na sasa anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Juventus baada ya hapo awali kuashiria nia yake ya kuondoka katika klabu hiyo, kama ilivyoripotiwa na Tuttosport.

Mkutano wa mazungumzo ya mkataba mpya kati ya bodi ya wakurugenzi wa Juventus na mwakilishi wa Rabiot ambaye ni mama yake mzazi, Veronique, umepangwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Mtendaji Mkuu wa Man United, John Murtough hapo awali alisafiri kwa ndege hadi Turin kukutana naye katika harakati za kumnasa Rabiot ili atue pale Old Trafford, lakini ilishindikana.

Mama wa mchezaji hu
wakala wake na ana ufu
wa mkataba wowote mpy
baye ameshinda mataji n
is Saint-Germain na Juven

Juventus wanalenga
sainisha Rabiot kwa mk
wa miaka mitatu am
itaendelea hadi 2027 ili
tunza mchezaji huyo wa
taifa wa Ufaransa am
amekuwa na mwanzo n
wa msimu mpya.

Klabu hiyo ina nia ya
baliana mkataba mpya n
biot kabla ya Januari kuto
na mchezaji huyo kuwez
fikia makubaliano ya awa
mkataba na timu nyingine



# TWIGA STARS YAKABIDHIWA MILIONI 10/- BAO LA MAMA

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amewataka wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kuendelea kupambana katika mashindano yaliyopo mbele yao ili kuitangaza vizuri Tanzania.

Amesema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, anataka Watanzania wafurahi na ili kuwafurahisha ni kufanya vizuri katika mashindano yaliyopo mbele yao ikiwamo Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON) na kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia.

Msigwa alitoa kauli hiyo katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana baada ya mazoezi ya timu hiyo kwenye hafla fupi ya kuwakabidhi kitita cha Sh. milioni 10 zilizotolewa na Rais Samia kama motisha kutokana na ushindi walipata dhidi ya Ivory Coast.

> **Alisema wachezaji hao wanafanya kazi kubwa ya kuiwakilisha nchi kimataifa na serikali ipo pamoja nao kwa kuwa wanaitangaza na kuipigania nchi yao.**

"Mnapokuwa uwanjani katika mechi za kimataifa mnakuwa mmebeba matumaini ya Watanzania, katika mechi zote mlizocheza tumeona dhamira mliyonayo kwa nchi yenu, Rais Samia anawapongeza na anafurahi sana anapowaona mnacheza uwanjani, anafurahi sana mnapopata matokeo mazuri katika mechi zenu," alisema Msigwa.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema amefurahi kupokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Mama Samia kwa ajili ya kuhamasisha vijana hao kujituma zaidi kupambania nchi yao, lakini kubwa kwa vijana hao kuona rais anatambua mchango wao.

"Fedha ni sehemu kubwa ya hamasa, kitendo cha Rais Samia kuwafuatilia vijana wetu na kutambua timu hiyo inacheza, ni faraja kubwa kwao na imekuwa chachu ya kujituma wakiamini kuwa mama yupo pamoja nao," alisema Shime.

Naye Nahodha wa Twiga Stars, Joyce Lema, alisema wanamshukuru Rais Samia kwa kuzidi kuwapa hamasa na kumuahidi kutomwangusha katika mashindano yote yaliyopo mbele yao.

"Kwa hamasa hii inaonesha kuwa kuna kitu kimeongezeka katika soka la wanawake, tunatamani siku moja viongozi kuendelea kujitokeza kwa wingi kusapoti soka la wanawake kama ilivyo kwa wanaume," alisema Joyce.



Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, akimkabidhi nahodha wa Timu ya Twiga Stars, Joyce Lema, kitita cha Sh. milioni 10 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni motisha kutokana na ushindi walioupata dhidi ya Ivory Coast. Makabidhiano hayo yalifanyika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Robertinho na 'sab' ya Bocco

INATOKA UK. 24

kufikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimbazi.

"Niwaombe tu mashabiki na wadau wa Simba kuwa na uvumilivu kwa kuwa siku zote hatutakuwa na mechi rahisi, kwa sababu tumecheza na timu ngumu sana, lakini wasikate tamaa na waendelee kutoa sapoti kwa benchi la ufundi kwenye mabadiliko anayoyafanya," alisema.

Naye Kocha wa Power Dynamos, Mwenya Chipepo, alisema wamekosa bahati kwa sababu wamecheza vizuri kipindi cha kwanza ambacho walitawala mchezo kwa dakika 45.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia na kupata bao la kwanza na Simba kufanikiwa kusawazisha bao hilo baada ya makosa waliyofanya walinzi wake.

"Niwapongeze Simba, lakini wanatakiwa wafanye kazi baada ya kufuzu makundi kwa sababu wameingia hatua ngumu, tumepokea matokeo na tunaenda kujiandaa na ligi ya nyumbani," alisema Chipepo.

## *Simba, Yanga zanukia kukutana makundi CAF*

INATOKA UKURASA 24

tano.

Endapo Simba na Yanga zitapangwa kundi moja, itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya michuano CAF kupigwa 'Dabi Kariakoo' kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imefuzu hatua ya makundi baada ya kuitoa Power Dynamos kwa faida ya bao la ugenini kutokana na kutoka sare ya mabao 2-2 nchini Zambia kabla ya juzi kutoka tena sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kwa upande wa Yanga yenyewe ilitoa Al-Merrikh ya Sudan kwa jumla ya mabao 3-0 baada ya kushinda 2-0 ugenini na kisha nyumbani kuichapa bao 1-0.


# 573,060 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/10/23 | 22:00 | Newcastle vs Paris St Germain | 2.39 | 3.52 | 2.58 |
| 02. 04/10/23 | 22:00 | Celtic vs Lazio | 2.73 | 3.43 | 2.31 |
| 03. 04/10/23 | 22:00 | Borussia Dortmund vs AC Milan | 2.30 | 3.47 | 2.73 |
| 04. 04/10/23 | 22:30 | Burgos vs Leganes | 2.37 | 2.97 | 3.02 |
| 05. 04/10/23 | 22:30 | Sporting Gijon vs Elche | 2.53 | 3.12 | 2.68 |
| 06. 05/10/23 | 16:00 | Mtibwa Sugar vs Singida BS FC | 2.48 | 2.94 | 2.89 |
| 07. 05/10/23 | 19:45 | Marseille vs Brighton | 2.80 | 3.55 | 2.27 |
| 08. 05/10/23 | 19:45 | SC Freiburg vs West Ham | 2.49 | 3.43 | 2.58 |
| 09. 05/10/23 | 19:45 | Sporting Lisbon vs Atalanta | 2.22 | 3.36 | 3.01 |
| 10. 05/10/23 | 19:45 | Rakow Czestochowa vs Sturm Graz | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 11. 05/10/23 | 22:00 | BK Hacken vs Karabakh | 2.47 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 05/10/23 | 22:00 | Maccabi Haifa vs Panathinaikos | 2.25 | 3.36 | 2.96 |
| 13. 05/10/23 | 22:00 | PAOK vs Eintracht Frankfurt | 2.70 | 3.36 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 03/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3021 | Ural Yekaterinburg vs Rubin Kazan | 2.09 | 3.22 | 3.22 |
| 16:00 | 2670 | JKT Tanzania vs Mashujaa FC | 2.04 | 3.26 | 3.41 |
| 17:00 | 5850 | Torpedo Kutaisi vs Saburtalo Tbilisi | 2.55 | 3.20 | 2.42 |
| 17:15 | 2150 | Zenit St Petersburg vs Baltika Kaliningrad | 1.33 | 4.88 | 6.92 |
| 17:15 | 5705 | Lokomotiv Moscow vs Rostov | 1.57 | 3.91 | 4.78 |
| 18:35 | 5560 | Ohud Medina vs AL Jandal | 2.02 | 2.95 | 3.50 |
| 18:35 | 5587 | AL Khlood vs AL Ain | 2.06 | 2.97 | 3.48 |
| 19:00 | 4884 | Dodoma FC vs Azam | 4.15 | 3.21 | 1.86 |
| 19:00 | 5873 | Dinamo Tbilisi vs Dila Gori | 1.64 | 3.65 | 4.20 |
| 19:45 | 3884 | Bordeaux vs Caen | 2.19 | 3.23 | 3.09 |
| 19:45 | 4544 | Union Berlin vs Sporting Braga | 1.83 | 3.51 | 3.86 |
| 19:45 | 4781 | RB Salzburg vs Real Sociedad | 2.68 | 3.23 | 2.45 |
| 20:00 | 1448 | Alcorcon vs Albacete Balompie | 2.53 | 3.12 | 2.68 |
| 20:00 | 1667 | Gefle IF vs Orgryte IS | 3.18 | 3.44 | 2.15 |
| 20:00 | 3072 | Gais vs Osters IF | 2.11 | 3.40 | 3.30 |
| 20:00 | 3679 | Landskrona Bois vs GIF Sundsvall | 1.92 | 3.61 | 3.66 |
| 20:00 | 3825 | SSV Ulm vs 1860 Munich | 2.34 | 3.47 | 2.74 |
| 20:00 | 4684 | Helsingborg vs Orebro SK | 2.73 | 3.30 | 2.50 |
| 20:30 | 4897 | Kaizer Chiefs vs Cape Town City | 1.99 | 3.02 | 3.89 |
| 21:30 | 5018 | Luton Town vs Burnley | 2.74 | 3.26 | 2.64 |
| 21:45 | 1491 | Bolton vs Stevenage | 2.04 | 3.45 | 3.35 |
| 21:45 | 1579 | Burton vs Wigan | 2.56 | 3.36 | 2.56 |
| 21:45 | 1875 | Plymouth vs Millwall | 2.37 | 3.41 | 2.67 |
| 21:45 | 1876 | Northampton vs Reading | 2.48 | 3.41 | 2.61 |
| 21:45 | 2144 | Cambridge Utd vs Barnsley | 2.81 | 3.41 | 2.32 |
| 21:45 | 2412 | Carlisle vs Peterborough | 3.21 | 3.56 | 2.05 |
| 21:45 | 2766 | Birmingham vs Huddersfield | 2.13 | 3.18 | 3.28 |
| 21:45 | 3009 | Cheltenham vs Fleetwood Town | 2.96 | 3.36 | 2.25 |
| 21:45 | 3020 | Gateshead vs Wealdstone | 1.46 | 4.55 | 5.58 |
| 21:45 | 3392 | Leyton Orient vs Lincoln | 2.10 | 3.36 | 3.26 |
| 21:45 | 3793 | Charlton vs Exeter | 2.01 | 3.51 | 3.36 |
| 21:45 | 3822 | Middlesbrough vs Cardiff | 1.77 | 3.51 | 4.16 |
| 21:45 | 3869 | Portsmouth vs Wycombe | 1.74 | 3.55 | 4.49 |
| 21:45 | 4587 | Newport vs Colchester | 2.06 | 3.44 | 3.10 |
| 21:45 | 4656 | Crewe vs Gillingham | 2.59 | 3.13 | 2.54 |
| 21:45 | 4765 | Harrogate vs AFC Wimbledon | 2.85 | 3.29 | 2.25 |
| 21:45 | 5422 | Bristol Rovers vs Port Vale | 2.00 | 3.45 | 3.45 |
| 21:45 | 5790 | Ipswich vs Hull City | 1.62 | 3.86 | 4.65 |
| 21:45 | 5802 | Woking vs Halifax | 1.83 | 3.30 | 4.23 |
| 21:45 | 5931 | Oxford Utd vs Shrewsbury | 1.55 | 3.90 | 5.60 |
| 21:45 | 5987 | Blackpool vs Derby | 2.29 | 3.35 | 2.90 |
| 22:00 | 1381 | PSV Eindhoven vs Sevilla FC | 1.93 | 3.48 | 3.53 |
| 22:00 | 1995 | Napoli vs Real Madrid | 2.53 | 3.47 | 2.47 |
| 22:00 | 2107 | Inter vs Benfica | 1.74 | 3.65 | 4.15 |
| 22:00 | 3138 | West Bromwich vs Sheffield Wed | 1.60 | 3.62 | 5.35 |
| 22:00 | 4017 | Stoke City vs Southampton | 2.58 | 3.37 | 2.47 |
| 22:00 | 4171 | Copenhagen vs Bayern Munchen | 10.29 | 6.17 | 1.20 |
| 22:00 | 4466 | Manchester Utd vs Galatasaray | 1.42 | 4.49 | 6.13 |
| 22:00 | 4583 | Lens vs Arsenal | 5.14 | 4.05 | 1.54 |
| 22:30 | 1813 | Tenerife vs Racing Santander | 1.83 | 3.23 | 4.28 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Jumanne Oktoba 3, 2023

Nipashe




Martinez apasuliwa tena

UKURASA 21




Gamondi

Robertinho

# Simba, Yanga zanukia kuvaana makundi CAF

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Droo kuamua Ijumaa Afrika Kusini, zote mdomoni mwa Al Ahly, Wydad, Mamelodi na...

MIAMBA ya soka na watani wa jadi nchini, Simba na Yanga itajua timu itakazokutana nazo katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye droo itakayochezeshwa Ijumaa wiki hii jijini Johannesburg, Afrika Kusini huku kukiwa na uwezekano wa zenyewe kukutana katika kundi moja.

**Tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limepanga timu zote 16 katika pot namba moja hadi nne kulingana na pointi ya kila timu ilizovuna kwa kipindi cha miaka mitano huku Simba yenye pointi 29 ikiwa Pot 2 na Yanga yenye pointi 21 ikiwa Pot 3.**

Droo hiyo inajumuisha jumla ya timu 16 zilizofuzu michuano hiyo kwa kupangwa nne nne kila pot ili kuchakata kupata makundi manne ambapo kila kundi litakuwa na timu nne pia.

Ikumbukwe timu zilizo katika pot moja haziwezi kukutana kwani kila pot huchukuliwa timu moja kwenda kuunda kundi moja na timu tatu tofauti kutoka katika kila pot, hivyo Simba na Yanga zinaweza kupangwa kundi moja kwa kuwa zipo pot tofauti.

Simba inaweza kupangwa kundi moja na timu yoyote kutoka Pot namba moja, tatu na nne, wakati Yanga nayo inaweza kupangwa kundi moja na timu kutoka Pot namba moja, mbili na nne.

Pot 1lina vigogo bora vya soka Afrika kwa sasa; Al Ahly ya Misri yenye pointi 62, Wydad ya Morocco (54), Esperance ya Tunisia (41) na Mamelodi ya Afrika Kusini yenye pointi 39.

Pot 2 zimo CR Belouizdad ya Algeria yenye pointi (32), Simba ya Tanzania (29), Petro de Luanda ya Angola (29) na Pyramids ya Misri (29).

Hata hivyo, kuwapo kwa CR Belouizdad kwenye pot hilo itategemea kama jana usiku ilifuzu kwani ilitarajia kuikaribisha Bo Rangers FC ya Sierra Leone katika mchezo wa marudiano baada ya ule wa awali ugenini kushinda kwa mabao 3-0.

Pot 3 linaundwa na TP Mazembe ya DR Congo yenye pointi 23, Yanga ya Tanzania (21), Asec Mimosas ya Ivory Coast (20) na Al Hilal ya Sudan (20).

Pot 4 zimo Etoile Saleh ya Tunisia yenye pointi 16, Jwaneng Galaxy ya Botswana (8), FC Nouadhibou ya Mauritania (5.5) na Medeama SC ya Sierra Leone yenye pointi

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho na 'sab' ya Bocco

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufuzu kwa mbinde hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema kikubwa ni timu yake imevuka kucheza hatua hiyo kwani walikutana na mpinzani mgumu.

Amesema kwa kiasi kikubwa benchi la ufundi na wachezaji wamefurahi kuingia hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kujiandaa na yaliyopo mbele yao ili kufikia malengo.

Simba imefuzu hatua ya makundi baada ya kuitoa Power Dynamos kwa faida ya bao la ugenini kutokana na kutoka sare ya mabao 2-2 nchini Zambia kabla ya juzi kutoka tena sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe baada ya kukamilika kwa dakika 90 juzi, Robertinho alisema lengo la kwanza lilikuwa kuhakikisha timu inaingia hatua ya makundi kwa kuitoa Power Dynamos na hilo limefanikiwa.

Aliwapongeza wachezaji kwa kutokata tamaa hadi mwisho akidai Power Dynamos ni timu bora na ilikuwa imejipanga vizuri kwa michezo yote miwili ya nyumbani na ugenini.

Kuhusu kumwingiza John Bocco aliyesababisha kupatikana kwa bao la kusawazisha, Robertinho alisema: "Nilifanya mabadiliko hayo kipindi cha pili kwa kuwa niliwaona Dynamos wote wamerudi nyuma na waliziba mianya ya kupitisha pasi, alitakiwa mtu wa kusimama na mabeki wao na aliende kufanya kazi niliyomtuma.

"Baada ya Power Dynamos kupata bao, walirudi nyuma wote ikawa ngumu kupitisha mipira ikabidi tumwingize Bocco kwa kuwa ni mrefu angeweza kucheza sambamba nao tulionge kasi iliyosababisha kupatikana kwa bao la kusawazisha," alisema kocha huyo.

Kiungo wa Simba, Said Ntibazonkiza, alisema mechi ilikuwa ngumu na walipambana kwa dakika zote na kufanikiwa kufuzu na kucheza hatua ya makundi.

Alisema mechi imeisha wanaangalia zaidi yaliyopo mbele kuendelea kupambania timu kufanya vizuri na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >